# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# MKAKATI WA TAIFA WA KONDOMU

**2019 - 2023**

**Agosti, 2019**

## SHUKURANI

Mkakati wa Taifa wa Kondomu 2019–2023 umetayarishwa na Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS), kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto (MoHCDGEC) kufuatia mkakati wa kondomu wa mwaka 2016-2018 kumalizika muda wake. TACAIDS inatoa shukurani za dhati kwa wadau na Taasisi zilizoshiriki katika mchakato wa utayarishaji wa mkakati huu, wadau na taasisi hizo ni pamoja na Serikali Kuu na Serikali za Mitaa, Asasi za Kiraia na Kijamii, Sekta binafsi, na Wabia wa maendeleo.

TACAIDS inatoa shukurani za dhati kwa michango ya wawakilishi wa taasisi zifuatazo:

- Wizara, Idara zinazojitegemea na Wakala za Serikali (MDAs): Ofisi ya Rais–Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora (OR-MUUUB); Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI); Ofisi ya Makamu wa Rais; Ofisi ya Waziri Mkuu–Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu; Wizara ya Fedha na Mipango; Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi; Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari; Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa, na Michezo; Wizara ya Mifugo na Uvuvi; Wizara ya Elimu, Sayansi, na Teknolojia; Wizara ya Viwanda na Biashara; Wizara ya Madini; Wizara ya Sheria na Katiba; Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; Wizara ya Maji; Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa; Wizara ya Mambo ya Ndani; Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki; Wizara ya Kilimo; Sekretarieti ya Tawala za Mikoa na Halmashauri ya Jiji la Dodoma.

- Shukurani ziwaendee wadau muhimu wa mwitikio wa Mkakati wa kondomu kutoka USAID, UNFPA, UNAIDS, DOD –WRAIR, MSD, TMDA, TBS, NACOPHA, SHOPS PLUS, PSI, T-MARC, TAYOA, AMREF, FHI360, JSI, JHIEGO, NYP+, DKT, ATE, Duka la Dawa la JD, Belva Consulting Limited, General De-Pharmacy na APHFTA.

- Pia, tunawashukuru Kamati ya Kitaalamu ya kudhibiti UKIMWI; Kamati Shirikishi ya Kondomu ya Taifa; Kamati ya Kitaalamu ya Ufuatiliaji, Tathmini na Utafiti, pamoja na Mtaalamu Elekezi: Dkt. Patrick Kanyamwenge ambaye alitayarisha mkakati huu kufuatia ushauri na mwongozo kutoka kwa wadau.

Shukurani za pekee ziwaendee Mfuko wa Dunia wa kudhibiti UKIMWI, Malaria na Kifua Kikuu (GFATM) kwa msaada wao wa kifedha katika kipindi chote cha utayarishaji na ukamilishaji wa mkakati huu.

Dr. Leonard L. Maboko

**Mkurugenzi Mtendaji**

**Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS)**

**DIBAJI**

Janga la VVU na UKIMWI limekuwa tishio na linaathiri ngazi zote nchini, kuanzia ngazi ya Kijiji hadi ya Taifa. Kwa zaidi ya miongo mitatu sasa Serikali ya Tanzania imefanya maboresho makubwa kama mwitikio katika kupunguza maambukizi ya janga la VVU, ikiwa ni pamoja na kuboresha Tiba ya Kuongeza Kinga ya Mwili (ART) na uratibu wa kuzuia maambukizi ya VVU. Vilevile, Serikali imejikita katika kutekeleza mkakati wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Kudhibiti UKIMWI (UNAIDS) katika kutokomeza janga la UKIMWI ifikapo mwaka 2030, na kuupa kipaumbele mkakati wa 90-90-90, ambapo asilimia 90 ya watu wanaoishi na VVU kujua hali zao za maambukizi, asilimia 90 ya wanaojua hali zao kuanzishiwa na kuendelea kupata tiba na asilimia 90 ya wagonjwa walio katika tiba kufanikiwa kupunguza makali ya virusi vya UKIMWI ifikapo mwaka 2020.

Hivyo, umuhimu wa kupitia na kutathmini Mkakati wa Taifa wa Kondomu unadhihirika kupitia upungufu katika eneo la sera, uratibu, ugavi, usambazaji na upatikanaji wa kondomu uliobainishwa wakati wa uchambuzi wa nyaraka muhimu za kitaifa, pamoja na majadiliano na wadau kutoka ngazi zote. Masuala muhimu yaliyoibuliwa wakati wa uchambuzi ni pamoja na uwezo mdogo wa kifedha katika kukidhi mahitaji ya kondomu, usambazaji na ufuatiliaji hafifu pamoja na kukosekana kwa uendelevu wa programu za kondomu nchini. Licha ya changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa mkakati wa kondomu kwa kipindi cha miaka miwili ya utekelezaji wake; (kutoka mwaka 2016 hadi mwaka 2018), Serikali ilifanikiwa kusambaza zaidi ya kondomu za kiume milioni 249, ambapo kondomu milioni 49 kati ya hizo zilisambazwa kupitia sekta za umma, na kondomu zaidi ya milioni 200 zilisambazwa kupitia masoko ya kijamii, pamoja na sekta za kibiashara.

Juhudi za Serikali katika kuzuia maambukizi mapya ya VVU zimelenga makundi maalumu na yaliyoko katika mazingira hatarishi, wakiwemo wasichana balehe na wanawake vijana walio katika mazingira hatarishi zaidi, wanaume wanaoshiriki ngono na wanaume wenzao, wanawake wanaofanya biashara ya ngono, watu wanaojidunga dawa za kulevya, watu wanaotumia dawa za kulevya. Wengine ni wafungwa magerezani, wafanyakazi wa migodini, na wengineo. Hivyo ni lazima kuwapo na ongezeko katika kiwango cha matumizi ya kondomu kama njia thabiti dhidi ya VVU, na maambukizi mengine kupitia ngono na mimba zisizotarajiwa. Ili kuchochea ongezeko la kiwango cha matumizi ya kondomu kwa wanaozihitaji, Mkakati huu wa Kondomu umetayarishwa kwa lengo la kuhakikisha kunakuwa na matumizi sahihi na endelevu ya kondomu kwa ajili ya kudhibiti VVU, maambukizo kupitia ngono, pamoja na kuzuia mimba zisizotarajiwa na zile za mapema nchini. Pia, mkakati utachangia kuondoa fikra zisizo sahihi zinazosababisha uhatarishi kupitia

utoaji wa elimu jamii na uhamasishaji. Lengo ni kuleta mabadiliko chanya ya kutoka katika uelewa usio sahihi juu ya VVU na UKIMWI na kwenda kwenye uelewa sahihi, ambapo walengwa wataweza kutambua tabia hatarishi za kingono na hivyo kuchukua hatua stahiki. Mafanikio na uendelevu wa utekelezaji wa Mkakati wa Kondomu yamejikita kwenye ushirikishwaji wa wadau wote wa kondomu, wakiwamo; Serikali, Asasi za Kiraia na kijamii, sekta binafsi, Wabia wa Maendeleo, pamoja na wanajamii. Kwa uratibu wa TACAIDS, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, kupitia Mpango wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI na Huduma za Afya ya Uzazi na Mtoto itatoa maelekezo muhimu juu ya utekelezaji wa mkakati huu. Bohari Kuu ya Dawa itaendelea na utaratibu wa usimamizi wa manunuzi na usambazaji, na Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba, itasimamia ubora wa kondomu katika sekta zote. Mwisho, inatarajiwa kuwa wadau wa kitaifa na kimataifa wataendelea kutimiza majukumu yao katika utoaji wa msaada wa kitaalamu na kifedha pindi itakapohitajika. Pia, inatarajiwa kuwa, mkakati huu sambamba na miongozo mingine ya kitaifa ya VVU na UKIMWI, na afya ya uzazi itatokomeza janga hili la UKIMWI, pamoja na maambukizi mengine ya magonjwa ya ngono na mimba zisizotarajiwa.

**Prof. Abel Makubi**

**Katibu Mkuu**

**Wizara ya Afya**

**YALIYOMO**

**SHUKURANI** .......... ii
**DIBAJI** .......... iv
**YALIYOMO**.......... vi
**ORODHA YA MAJEDWALI** .......... viii
**ORODHA YA VIELELEZO** .......... viii
**VIFUPISHO** .......... ix
**MUHTASARI RASMI** .......... xii
**SEHEMU YA 1: USULI** .......... 1
**1.2 Sera ya Kondomu** .......... 2
**1.2.1 Mkakati wa Kondomu**.......... 3
**1.3 Dhana ya Mfumo wa Masoko Jumuishi ya Kondomu**.......... 5
**1.4 Mchakato wa utayarishaji wa Mkakati wa Kondomu**.......... 6
**SEHEMU YA 2: UCHAMBUZI**.......... 8
**2.1 Matokeo ya mapitio ya nyaraka na vikao vya ushauri vya uchambuzi wa taarifa na**.......... 8
**takwimu.**.......... 8
2.1.1 Matumizi ya Kondomu Nchini Tanzania.......... 8
**2.2 Ulinganifu waTanzania Katika Nchi za Mashariki na Kusini mwa Afrika** .......... 10
**2.3 Uchambuzi wa Masoko** .......... 11
2.3.1 Wadau/wahusika katika soko la kondomu.......... 11
2.3.2 Usambazaji endelevu wa kondomu .......... 14
2.3.3 Upana wa/ Kina cha Soko.......... 15
**2.4 Vikwazo/vizuizi katika matumizi ya kondomu**.......... 16
2.4.1 Fursa katika ufikiaji wa kondomu.......... 16
2.4.2 Uelewa/uwezo wa kutumia au kujadiliana kuhusu matumizi ya kondomu.......... 16
2.4.3 Upatikanaji wa kondomu .......... 17
2.4.4 Mitazamo na Fikra/imani.......... 18
**2.5 Tofauti kuu za kijiografia katika upatikanaji wa kondomu** .......... 18
**2.6 Uwepo wa sekta mahususi** .......... 18
**2.7 Uelewa juu ya chapa/aina ya kondomu kulingana na mgawanyo wa Mfumo wa Masoko ya Jumuishi**.......... 19
**2.8 Mafanikio na changamoto kuu katika uratibishaji wa programu za kondomu**.......... 19
**SEHEMU YA 3: LENGO, DHUMUNI, MATOKEO NA MIONGOZO ELEKEZI** .......... 28
**3.1 Lengo** .......... 28
**3.2 Dhumuni** .......... 28
**3.3. Matokeo ya kimakakati**.......... 28
**3.4 Kanuni elekezi** .......... 29
**SEHEMU YA 4: MIKAKATI YA UTEKELEZAJI** .......... 31
**4.1 Uboreshaji wa Uongozi na Uratibu.** .......... 31
4.1.1 Uratibu wa Wadau .......... 31
4.1.2 Uraghibishaji wa Rasilimali.......... 32
**4.2 Uboreshaji wa usambazaji na uhakika wa bidhaa** .......... 33
4.2.1 Mpango wa makisio ya usambazaji wa kondomu. .......... 33
4.2.2 Mfumo wa Usimamizi wa Taarifa .......... 34
4.2.3 Kuongeza usambazaji wa kondomu kupitia mitandao ya sekta binafsi, masoko ya kijamii, na sekta za biashara .......... 34
**4.3 Uhitaji, Upataji na Utumiaji** .......... 35
4.3.1 Usambazaji wa Kondomu kwa walengwa .......... 35

4.3.2 Mfumo wa Masoko ya Jumuishi katika kuongeza kiwango cha upataji wa kondomu........ 37
4.3.3 Utekelezaji wa Mfumo wa Masoko Jumuishi: Majukumu na Wajibu katika ngazi mbalimbali ........................................................................................................ 37
4.3.4 Mawasiliano ya Mabadiliko ya Tabia katika Jamii kwa ajili ya matumizi ya kondomu.. 39
**4.4 Majukumu ya mipango ya programu na Msaada ........................................................ 41**
4.4.1 Tafiti, Ufuatiliaji na Tathmini......................................................................................... 41
**SEHEMU YA 5: PROGRAMU ZA KONDOMU ZA KIKE NA AFUA ZA KIMKAKATI ..................................................................................................................... 42**
**5.1 Utangulizi........................................................................................................................ 42**
**5.2 Vikwazo katika kuongeza kiwango cha matumizi ya kondomu ya kike ........................ 43**
**5.3 Mikakati ya kuongeza kiwango cha matumizi ya kondomu ya kike.............................. 44**
5.3.1 Nafasi ya Kondomu ya Kike.............................................................................................. 44
5.3.2 Makundi Maalumu na Yaliyobainiwa ............................................................................. 44
5.3.3 Njia mbalimbali za utoaji huduma na usambazaji .......................................................... 44
5.3.4 Uimarishaji wa muunganisho wa Kondomu za Kike ...................................................... 44
5.4.5 Kuandaa mikakati bunifu ya uhamasishaji ..................................................................... 44
5.4.6 Kutoa mafunzo kwa watoa huduma.................................................................................. 44
5.4.7 Kufanya uraghibishaji wa Wadau Muhimu ..................................................................... 45
5.4.8 Kufanya Tafiti endeshaji za pamoja ................................................................................ 45
5.4.9 Kuandaa Msaada wa kitaalamu na kifedha...................................................................... 45
**SEHEMU YA 6: MAJUKUMU NA WAJIBU WA WADAU MUHIMU.............................. 46**
**6.1 Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS).......................................................... 46**
**6.2 WIZARA, IDARA ZINAZOJITEGEMEA NA WAKALAWA SERIKALI ................... 46**
**6.3 Wizara ya Afya , Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ...................................... 47**
**6.4 Elimu na Mafunzo ya Ufundi ........................................................................................... 47**
**6.5 Wizara ya fedha na Mipango.............................................................................................. 48**
**6.6 Mamlaka ya Serikali za Mtaa............................................................................................. 48**
**6.7 Wizara zingine, pamoja na Idara Zinazojitegemea Wakala za Serikali ........................... 48**
6.8 Utafiti na Taasisi za Elimu ya Juu ...................................................................................... 49
**Taasisi za Elimu ya Juu zinawajibika ipasavyo katika Mwitikio wa taifa wa VVU na UKIMWI, kupitia muongozo wa kitaalamu, tafiti na mafunzo ya wataalamu wa baadae. Ujumuishaji wa maarifa kuhusu matumizi ya kondomu katika mipango anuai yakitaaluma inapaswa kutekelezwa.................................................... 49**
**6.9 Sekta binafsi rasmi na zisizo rasmi..................................................................................... 49**
6.10 Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba ..................................................................................... 49
**6.11 Wabia wa Maendeleo......................................................................................................... 49**
**6.12 Asasi za Kiraia na Kijamii ................................................................................................ 49**
**6.13 Shirika la Sekta Binafsi ya Afya Tanzania......................................................................... 50**
**REFERENCES........................................................................................................................ 51**
**KIAMBATISHO CHA 1: Kiwango cha kondomu zinazohitajika Tanzania 2019-2020...... 53**

## ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali la 1: Uelewa juu ya matumizi ya Kondomu kama njia ya uzazi wa mpango……27
Jedwali la 2: Kiwango cha matumizi ya kondomu miongoni mwa makundi rika mbalimbali…………………………………………………………………31
Jedwali la 3: Aina/chapa za kondomu zinazopendwa zaidi…………………………………35
Jedwali la 4: Mfumo wa jumuishi wa kuratibu programu za kondomu ……………………47
Jedwali la 5: linaonyesha makadilio ya idadi ya kondomu zinazohitajika Tanzania mwaka 2019-2020……………………………………………………………………...72

## ORODHA YA VIELELEZO

Kielelezo cha 1: Kiasi cha Usambazaji wa Chapa/aina za Kondomu ....................................32
Kielelezo cha 2: Kondomu zilizosambazwa na Wadau wa masoko......................................34

**VIFUPISHO**

| | |
|---|---|
| ADDO | Mpango wa Kuboresha Maduka ya Dawa Baridi Nchini |
| AMREF | Shirika la Kimataifa la Utafiti wa Tiba na Afya |
| APHFTA | Shirikisho la Vituo Binafsi vya Afya Tanzania |
| ATE | Chama cha Waajiri Tanzania |
| CBD | Wasambazaji wa Vifaa vya Afya na Uzazi wa Mpango |
| CBO | Asasi za Kijamii |
| CCP | Mpango wa Kina wa Matumizi ya Kondomu |
| CHF | Mfuko wa Afya wa Jamii |
| CHW | Watoa Huduma za Afya wa Jamii |
| CMAC | Kamati za Kudhibiti UKIMWI katika Mamlaka za Serikali za Mitaa |
| CSO | Asasi za Kiraia |
| DHS | Utafiti wa Demografia na Afya |
| DPs | Wabia wa Maendeleo |
| eLMIS | Mfumo wa Kielektroni wa Usimamizi wa Taarifa |
| FHI | Asasi ya Kimataifa ya Afya ya Familia |
| FP CIP | Mpango wa Utekelezaji wa Uzazi wa Mpango Uliothaminishwa |
| FSW | Wanawake Wanaofanya Biashara ya Ngono |
| GFATM | Mfuko wa Dunia wa kudhibiti UKIMWI, Malaria na Kifua Kikuu |
| GMP | Mfumo wa Ubora wa Uzalishaji |
| HBV | Virusi vya Homa ya Ini B |
| HCV | Virusi vya Homa ya Ini C |
| HPV | Virusi Vinavyoshambulia Mlango wa Kizazi |
| HSHSP | Mpango Mkakati wa Kudhibiti VVU NA UKIMWI wa Sekta ya Afya |
| HSV | Virusi Vinavyosababibisha magonjwa ya Ngono/Virusi vya Tutuko Homa |
| IEC | Habari, Elimu na Mawasiliano |
| IPs | Wabia wa Utekelezaji |
| ILS | Mfumo Jumuishi wa Taarifa |
| JHU | Chuo Kikuu cha John Hopkins |
| JHPIEGO | Programu katika Chuo Kikuu cha John Hopkins ya Elimu ya Kimataifa ya Wanawake na Uzazi |
| KVPs | Makundi Maalumu na Yaliyoko katika Mazingira Hatarishi |
| MACs | Kamati za Kudhibiti UKIMWI |

| | |
|---|---|
| MDA | Wizara, Idara Zinazojitegemea na Wakala za Serikali |
| MoHCDGEC | Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto |
| MSD | Bohari Kuu ya Dawa |
| MSM | Wanaume Wanaofanya Ngono na Wanaume Wenzao |
| NACOPHA | Baraza la Taifa la Watu Wanaoishi na VVU |
| NACP | Mpango wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI |
| NFPCIP | Mpango wa Taifa wa Utekelezaji wa Uzazi wa Mpango Uliohuishwa |
| NMCS | Mkakati wa Taifa wa Kondomu |
| NMSF IV | Mkakati wa Nne wa Taifa wa Kudhibiti VVU NA UKIMWI (2018/19-2022/23) |
| NHIF | Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya |
| NYP+ | Mtandao wa Vijana Wanaoishi na VVU |
| PMTCT | Uzuiaji wa Maambukizo ya VVU Kutoka kwa Mama kwenda kwa Mtoto |
| PWID | Watu Wanaojidunga Dawa za Kulevya |
| PWUD | Watu Wanaotumia Dawa za Kulevya |
| RMAC | Kamati ya ya Kudhibiti UKIMWI ya Mkoa |
| RCHS | Huduma ya Afya ya Uzazi na Mtoto |
| RNA | Tathmini ya Mahitaji ya Haraka |
| PSI | Shirika la Kimataifa Linalohudumia Jamii |
| SBCC | Mawasiliano ya Mabadiliko ya Tabia na Jamii |
| SHOPS PLUS | Mradi Kiongozi Katika Kuimarisha Ushiriki wa Sekta Binafsi katika Afya |
| STI | Maambukizo kwa Ngono |
| TACAIDS | Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania |
| TAYOA | Shirika la Vijana Tanzania |
| TOT | Mafunzo kwa Wakufunzi |
| TBS | Shirika la ViwangoTanzania |
| TDHS | Utafiti wa Demografia na Afya Tanzania |
| THIS | Utafiti wa Viashirio vya VVU NA UKIMWI Tanzania |
| THMIS | Utafiti wa Viashirio vya VVU NA UKIMWI na Malaria Tanzania |
| TMA | Mfumo wa Masoko JumuishiTMDA Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba, |
| T-MARC | Shirika la Masoko na Mawasiliano |
| UKIMWI | Upungufu wa Kinga Mwilini |
| UNFPA | Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu |
| UNAIDS | Shirika la Umoja wa Mataifa la Kudhibiti UKIMWI |
| USAID | Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Marekani |

| | |
|---|---|
| VCT | Unasihi na Upimaji wa Hiari |
| VVU | Virusi vya UKIMWI |
| WAVIU | Watu Wanaoishi na Virusi vya UKIMWI |

**MUHTASARI RASMI**

Mkakati wa Taifa wa Kondomu wa mwaka 2016-2018 ulifanyiwa mapitio kwa lengo la kuainisha vipaumbele vya kimkakati vinavyohitajika katika kutokomeza VVU, maambukizi kupitia ngono pamoja na mimba zisizotarajiwa. Mchakato wa mapitio ya Mkakati wa taifa wa kondomu wa mwaka 2016-2018 ulilenga kuwashirikisha wadau katika kutayarisha mkakati mpya wa taifa wa kondomu wa mwaka 2019-2023. Sambamba na hilo, mchakato huu ulihusisha wadau mbalimbali ukiongozwa na kuratibiwa na serikali ya Tanzania kupitia TACAIDS.

Mkakati huu unatumia mbinu ya masoko jumuishi katika programu za kondomu, ambapo Serikali ya Tanzania inasimamia soko lote la kondomu. Mkakati huu unakusudia kuboresha uongozi na uratibu, uhakika wa bidhaa na ugavi, mfumo wa kuongeza mahitaji na msaada kupitia kinga inayotokana na ushahidi, ufikiaji na kupatikana kwa gharama nafuu, mbinu jumuishi na mgawanyo wa madaraka, uhusishaji wa sekta mbalimbali na mbinu ya masoko jumuishi kwa uendelevu

- Mkakati unalenga kufikia kwa kina malengo ya programu za kondomu yanayotokana na Mkakati wa nne wa Taifa wa Kudhibiti VVU na UKIMWI wa mwaka 2018/2019-2022/2023 ifikapo mwaka 2023. Kwa mujibu wa takwimu za mwaka 2017, matumizi ya kondomu yaliyoripotiwa wakati wa kujamiiana kwa mara ya mwisho kwa watu wazima wenye wapenzi zaidi ya mmoja ambao wana umri kati ya miaka 15-49 yalikuwa yameongezeka hadi asilimia 34 kwa wanaume na asilimia 27.7 kwa wanawake. Aidha, inakadiriwa kuwa matumizi ya kondomu yataongezeka hadi asilimia 50 kwa mwaka 2020 na asilimia 95 ifikapo Mwaka 2023
- Matumizi ya kondomu yaliyoripotiwa wakati wa kujamiiana kwa mara ya mwisho kwa vijana wenye umri kati ya miaka 15-24 yameongezeka kutoka asilimia 42 kwa wanaume na asilimia 37 kwa wanawake, kwa mujibu wa takwimu za Mwaka 2016. Aidha, inatarajiwa kuongezeka hadi asilimia 60 kwa mwaka 2020, na asilimia 80 ifikapo mwaka 2023.
- Mwisho, matumizi ya kondomu yaliyoripotiwa wakati wa kujamiiana kwa mara ya mwisho kwa makundi yaliyoko katika hatari zaidi na wapenzi wao wa hivi karibuni yameongezeka kutoka asilimia 32 ya wastani wa takwimu zilizoripotiwa mwaka 2013. Aidha, inatarajiwa kuongezeka hadi asilimia 80 kwa mwaka 2020 na asilimia 100 kufikia mwaka 2023.

Vifuatavyo ni Vipaumbele vya kimakakati vitakayofanikisha malengo yaliyobainishwa hapo juu:

**Uboreshaji wa Uongozi na Uratibu: Uratibu kwa ubia:**

1. Kuimarisha kamati shirikishi za taifa za kondomu kwa kubainisha hadidu za rejea, kupanua wigo wa uanachama, kamati ya mpango kazi ya kila mwaka, pamoja na makadirio stahiki ya mapato na matumizi.
2. Kuhakikisha kwamba kupitia mifumo ya uratibu iliyopo, mahitaji ya kondomu, upokelewaji, usambazwaji pamoja na ripoti zinakuwa ndiyo vipaumbele vya ajenda ya kamati zote kuanzia ngazi ya mkoa hadi ya kijiji.
3. Kujenga ushirikiano na uhusiano mzuri wa kazi kati ya sekta ya afya na sekta zinginezo katika ngazi zote ikijumuisha uwianishaji na uratibu wa wabia wa utekelezaji ili kurahisisha zoezi la utekelezaji wa mkakati wa kondomu.
4. Kuridhia na kutekeleza kanuni za Mfumo wa Masoko Jumuishi zinazohusu programu za kondomu nchini Tanzania.
5. Kuyatumia matamasha ya dini na majukwaa ya viongozi wa siasa ili kushughulikia vipaumbele vya kimkakati ambavyo vimeainishwa kwenye Mkakati wa Nne wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI

**Uboreshaji wa Uongozi na Uratibu: uhamasishaji na ukusanyaji wa rasilimali**

**Vipaumbele vya kimkakati:**

1. Kuanzisha uchambuzi wa sera na sheria, pamoja na majadiliano yanayohusu programu za kondomu.
2. Kutambua na kuimarisha wahamasishaji wa kondomu katika nyanja ya kisiasa, kidini, na kijamii.
3. Kujenga ushirikiano na asasi za kiraia, sekta binafsi na zisizo rasmi pamoja na asasi zingine zilizo katika jamii.
4. Kuhakikisha kunakuwa na fedha pamoja na rasilimali za kutosha katika utekelezaji na usambazaji wa mkakati wa kondomu, sambamba na ununuzi wa kondomu kwenye masoko ya sekta ya umma na kijamii.

**Uimarishaji wa Usambazaji na Uhakika wa bidhaa: mipango ya makisio na usambazaji:**

Vipaumbele vya kimkakati:

1. Kuhakikisha kwamba mipango ya makisio na usambazaji wa kondomu unazingatia sekta zote pamoja na masoko ya kijamii, na sekta za biashara.

2. Kutambua uhitaji wa usambazaji wa kondomu kupitia utoaji halisi wa makisio ya uhitaji wa kondomu.
3. Kuunganisha mfumo wa masoko jumuishi katika ngazi zote za Kiserikali ili kufanikisha utoaji wa kondomu zilizo na ubora wa kiwango cha juu, kwa kuzingatia kondomu za sekta ya umma, kondomu zenye punguzo, pamoja na kukuza na kuendeleza upatikanaji wa kondomu za kibiashara.
4. Kuhakikisha kuwa utunzaji wa kumbukumbu na utoaji taarifa za kondomu unafanyika katika ngazi zote ikiwemo sekta ya masoko ya kijamii na sekta ya biashara.
5. Kuhakikisha kuwa wahudumu wa afya na rasilimali watu kutoka sekta na mashirika mengine wanakuwa na ujuzi katika ubainishaji wa mahitaji ya kondomu.

**Uimarishaji wa Usambazaji na Uhakika wa bidhaa: Mfumo wa Usimamizi wa Taarifa za Ugavi**

**Vipaumbele vya kimkakati:**

1. Kuimarisha na kukuza mfumo jumuishi wa taarifa za ugavi ili uweze kukusanya takwimu bora na za kutosha kwa ajili ya makisio ya matumizi na mahitaji ya kondomu.
2. Kuimarisha mfumo wa kielektroni wa usimamizi wa taarifa ili kuwezesha upatikanaji sahihi wa takwimu zinazohusu kondomu.
3. Kuimarisha usimamizi wa njia za usambazaji kondomu katika ngazi zote ili kuhakikisha upatikanaji na ufikiwaji wa kondomu kwa watu wenye uhitaji.
4. Kuwianisha mfumo wa ununuzi wa kondomu.

**Uboreshaji wa Usambazaji na Uhakika wa bidhaa: Kuongeza wigo wa usambazaji wa kondomu kupitia mitandao ya sekta za umma, masoko ya kijamii, na sekta za biashara.**

Vipaumbele vya kimkakati:

1. Kuhakikisha kwamba mbinu za usambazaji wa kondomu, uagizaji, uwasilishaji, uhifadhi na ripoti zinazohusu matumizi ya kondomu zinajumuishwa kwenye Mwongozo wa Taifa wa Usambazaji wa Kondomu.
2. Kuunganisha uwekezaji katika mawasiliano ya mabadiliko ya tabia na mienendo katika jamii /uhamasishaji wa matumizi ya kondomu ukilenga afya ya jamii.
3. Kuhakikisha upatikanaji wa kondomu kupitia mitandao/ njia zote za usambazaji.
4. Kuhakikisha uboreshaji wa ufikiaji wa kondomu na ujumuishaji wa sekta zote zinazojihusisha na usambazaji wa kondomu ikiwa ni pamoja na sekta za umma, masoko ya kijamii, na sekta za biashara.
5. Kutumia na kusimamia kanuni za Mfumo wa Masoko Jumuishi wakati wa kugawa na kusambaza kondomu kwa wadau wote wa usambazaji wa kondomu.

**Uhitaji,Ufikiaji na Utumiaji: Usambazaji mahususi wa kondomu**

**Vipaumbele vya kimkakati:**

1. Kuhakikisha usambazaji wa miongozo inayohusu ugawaji wa kondomu kwa wadau wote.
2. Kuzingatia utafiti wa masoko ili kubainisha mahitaji na vipaumbele miongoni mwa makundi lengwa yaliyo kwenye jamii, pamoja na yale yaliyo katika hatari Zaidi. Mfano; wasichana balehe na wanawake vijana, makundi ya vijana, wanawake wanaofanya biashara ya ngono, wanaume wanaofanya ngono na wanaume wenzao, watu wanaojidunga dawa za kulevya, watu wanaotumia dawa za kulevya, wafanyakazi wa migodini, na taasisi za elimu ya juu n.k.
3. Kuhakikisha ukuzaji wa uelewa juu ya kinga dhidi ya maambukizi ya VVU kwa makundi lengwa mbalimbali yaliyo katika jamii wakiwamo watu wenye ulemavu ili kuondoa mila na fikra potofu juu ya matumizi ya kondomu.
4. Kuimarisha usambazaji wa kondomu katika ngazi zote.
5. Kushirikisha Asasi za Kiraia, Mabaraza ya Wazee, WAVIU, na makundi ya rika na jinsi zote wasioishi na VVU kama vile, Vijana, wanawake na wanaume watu wazima ili kuongeza kiwango cha mahitaji ya matumizi ya kondomu.
6. Kuhamasisha uanzishwaji wa asasi za kibiashara katika jamii kwa uendelevu wa upatikanaji wa kondomu.
7. Kuhakikisha upatikanaji wa makasha au mashine za kuweka na kutolea kondomu katika sehemu mbalimbali.

**Uhitaji, Ufikiaji na Utumiaji: Mfumo wa masoko jumuishi katika kuongeza kiwango cha ufikiaji wa kondomu.**

**Vipaumbele vya kimkakati:**

1. Kuwezesha uratibu unaolenga sekta zote zinazojishughulisha na usambazaji wa kondomu zikiwemo sekta za umma, masoko ya kijamii, na sekta za biashara ili kuongeza kiwango cha matumizi ya kondomu kwa makundi lengwa.
2. Kutengeneza mazingira wezeshi ya upatikanaji wa kondomu kwa wahitaji wote.
3. Kuhakikisha utekelezaji wa kanuni za Mfumo wa Masoko Jumuishi zinazomwezesha kila muwajibikaji kuratibu juhudi za utekelezaji huku akitimiza malengo mahsusi ya afya.
4. Kuanzisha utafiti wa namna bora ya utendaji ili kupata taarifa za masoko kupitia takwimu rasmi na za masoko.

**Uhitaji, Ufikiaji na Utumiaji: Mawasiliano ya Mabadiliko ya Tabia katika Jamii**

**Vipaumbele vya kimkakati:**

1. Kuhamasisha utekelezaji fanisi wa ubainishaji wa mahitaji ya kondomu wenye uhakika katika ngazi zote kwa kuzingatia makundi lengwa na kuhakikisha matokeo sawia.
2. Kuhakikisha upatikanaji wa ushahidi unaopimika wa kiwango bora cha mahitaji na matumizi ya kondomu kama kigezo cha kuleta mabadiliko chanya ya kitabia
3. Kuimarisha utoaji habari na elimu kuhusu kondomu kwa vijana yakiwamo makundi maalumu na yaliyoko katika mazingira hatarishi ikiwa ni pamoja na watu wenye ulemavu,
4. Kuongeza kiwango cha matumizi sahihi na endelevu ya kondomu katika ngazi zote.
5. Kuchochea uhamasikaji wa jamii ili kutengeneza mazingira stahiki kwa kondomu za kike na kiume.
6. Kuhakikisha kunakuwa na uchambuzi wa watumiaji wa kondomu.
7. Kusambaza ujumbe unaowawezesha wanawake kuwa na uelewa juu ya kujadiliana kuhusu matumizi ya kondomu, mila, pamoja na matumizi sahihi na endelevu ya kondomu.
8. Kutoa maelezo juu ya mila na fikra potofu juu ya matumizi ya kondomu.
9. Kutumia majukwaa ya teknolojia na watu wenye ushawishi mkubwa katika jamii (Kutengeneza programu tumizi kupitia simu za mkononi, matangazo ya mtandaoni na mitandao ya kijamii ili kuongeza kiwango cha ufikiaji na utumiaji wa kondomu)
10. Kuhamasisha upatikanaji wa kondomu katika vyuo na taasisi za elimu ya juu (Vyuo vishiriki/vyuo vikuu)
11. Kuhusisha sekta binafsi, katika kuongeza upatikanaji wa kondomu kwenye masoko ya jamii na biashara.

**Programu wezeshi: Utafiti, Ufuatiliaji na Tathmini**

**Vipaumbele vya kimkakati:**

1. Kuboresha ufuatiliaji na tathmini ya programu za kondomu katika ngazi zote (ni lazima takwimu za kondomu ziwe kipaumbele katika kufanya uamuzi, kama vile mahitaji, vipaumbele, upatikanaji na usambazaji.
2. Kuimarisha utafiti ili kusaidia utekelezaji wa programu za kondomu
3. Kujenga uwezo miongoni mwa wajumbe wa kamati ya UKIMWI ili kuhakikisha utekelezaji wenye ufanisi wa programu za kondomu.

Ufanikishaji wa vipaumbele vya kimkakati vilivyobainishwa hapo juu utawezekana kwa jitihada za pamoja za wadau wote.

## SEHEMU YA 1: USULI

### 1.1 Utangulizi

Miongoni mwa vipaumbele vikuu vya Afya ya Jinsi na Uzazi kwa Serikali ya Tanzania ni pamoja na kuzuia maambukizi ya VVU, maambukizo kupitia ngono na kupunguza mimba zisizotarajiwa.

Kwa sasa Tanzania Bara inakabiliwa na janga sugu la VVU na UKIMWI. Inakadiriwa kuwa zaidi ya watu milioni 1.7 wanaishi na maambukizi ya VVU Nchini, ambapo takwimu kutoka kwenye utafiti wa tatu wa kupima viashiria vya UKIMWI (THIS-2003/4, THIS-2016/17). zinaonyesha kwamba kiwango cha maambukizi ya VVU kimeshuka kutoka asilimia 7.0 kwa mwaka 2003 hadi asilimia 4.7 kwa mwaka 2016 miongoni mwa watu wenye umri wa kati ya miaka 15-49. Hata hivyo, takwimu za sasa zimeonyesha kwamba kiwango cha maambukizi ya VVU kimeongezeka kwa asilimia 6.3 miongoni mwa wanawake ikilinganishwa na kiwango cha asilimia 3.4 miongoni mwa wanaume. Vilevile, kiwango cha maambukizi kimeripotiwa kuongezeka katika makundi madogo maalum kama ifuatavyo: Asilimia 36 ya watu wanaodunga dawa za kulevya, asilimia 25 kwa wanaume wanaofanya ngono na wanaume wenzao, asilimia 26 kwa wanawake wanaofanya biashara ya ngono, asilimia 22 kwa watu wanaotumia dawa za kulevya, pamoja na asilimia 6.7 kwa wafungwa magerezani. Sambamba na hayo, takwimu zinaonyesha kuwa kuna ongezeko kubwa la maambukizi ya VVU miongoni mwa vijana. Inakadiriwa kuwa kati ya maambukizi mapya ya VVU 81,000 kwa mwaka 2016, asilimia 43 ni kwa vijana wenye umri wa chini ya miaka 24, ambapo kati yao asilimia 80 yapo kwa wasichana. Vilevile, takwimu zinaonyesha kwamba maambukizi ya VVU miongoni mwa wanawake vijana wenye umri wa kati ya miaka 15-19 ni mara mbili zaidi ya wanaume wenye umri huohuo, na ni mara 3 zaidi kwa wanawake wenye umri kati ya miaka 20-24.

Vilevile, Tanzania imeripotiwa kuwa na kiwango cha juu cha virusi vya maambukizo kupitia ngono kama vile: Virusi vinavyosambazwa kupitia ngono vilengelenge (HSV-2), Virusi vinavyoshambulia via vya uzazi na kusababisha saratani ya shingo ya kizazi, na Virusi vya homa ya ini ambayo hayana tiba wala kinga stahiki[1]. Pamoja na kuwepo kwa uthibitisho wa kisayansi kwamba ufanisi kwenye kudhibiti maambukizo kupitia ngono unaendana na upunguzaji wa maambukizi ya VVU, huduma na usimamizi wa mambukizo kupitia ngono hasa miongoni mwa makundi maalumu yaliyo katika mazingira hatarishi bado upo chini.

[1] HSHSP IV-2017-2022

Inasemekana kuwa maambukizi ya VVU nchini yanasababishwa hasa na kuwepo kwa mapenzi ya jinsia moja ambayo yameshamiri kwa asilimia 80[2]. Tafiti zilizofanyika kuhusu njia za usambazaji wa maambukizi ya VVU Tanzania bara zinaonyesha kuwa, maambukizi mengi mapya ya VVU (asilimia 38.8) yanasababishwa na wenza walio katika ndoa, asilimia 28.9 wenza wasio katika mahusiano ya kudumu, asilimia 1.3 wafanyabiashara ya ngono, asilimia 8.7 wateja wa wafanyabiashara ya ngono, asilimia 3.3 wapenzi wa wateja wa wafanyabiashara ya ngono, asilimia 7.6 wapenzi wa watu wanaoshiriki ngono nje ya ndoa , asilimia 2.1 watu wanaojidunga dawa za kulevya, na asilimia 6.8 wanaume wanaoshiriki ngono na wanaume wenzao. Hivyo ni kipaumbele cha Mkakati wa Kudhibiti VVU Tanzania kupunguza maambukizi ya VVU kwa njia ya kujamiiana.

Matumizi ya kondomu ni moja kati ya mbinu bora inayoweza kutumika kupunguza maambukizi ya VVU. Tafiti za kisayansi zinaonyesha kwamba kondomu zinazotengenezwa kwa kutumia malighafi aina ya latex inakinga maambukizi ya VVU na maambukizo kupitia ngono kwa zaidi ya asilimia 80. Hivyo, matumizi ya kondomu kwa njia ya kujamiiana ni kigezo muhimu sana kwa Mkakati wa Kudhibiti VVU na UKIMWI Tanzania.

Matumizi sahihi na endelevu ya kondomu ni muhimu katika kuboresha njia za kisasa za uzazi wa mpango Nchini Tanzania. Njia hii inakadiriwa kuchangia asilimia 3.9 katika uzazi wa mpango, ambapo asilimia 14.6, wanatumia kondomu kama njia ya uzazi wa mpango ikilinganishwa na asilimia 2.4 ya wanawake walioolewa

### 1.2 Sera ya Kondomu

**Sera ya Taifa ya Kudhibiti VVU na UKIMWI ya mwaka 2001:** Sera hii inajumuisha lengo mahususi la kifungu 3.2a (iib) inayoorodhesha mojawapo ya afua zake kuwa ni *pamoja na ‘kuhamasisha ngono salama, kusubiri, Kutoshiriki ngono, pamoja na kutumia kondomu kulingana na uelewa zaidi wa mtu juu ya matumizi ya kondomu*’. Sera imetayarishwa na imetekelezwa kupitia Mkakati wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI.

**Mkakati wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI wa mwaka 2018/19 to 2022/23**: Mkakati huu unazingatia matumizi ya kondomu kama afua muhimu katika kudhibiti VVU na maambukizo kupitia ngono, pamoja na uzazi wa mpango. Vilevile, mkakati huu unalenga kupunguza maambukizi mapya kwa watu wazima wenye umri kati ya miaka 15-49. Moja kati ya afua muhimu katika kufikia lengo hili ni kuhamasisha uhitaji wa matumizi ya kondomu pamoja na kuongeza/kupanua uelewa unaohusu masuala ya maambukizi ya VVU miongoni mwa watu. Pia, mkakati huu unalenga kuhakikisha kwamba kunakuwa na ongezeko la usambazaji wa

[2] Spectrum,2013

kondomu katika maeneo lengwa na miongoni mwa makundi muhimu na yaliyo katika mazingira hatarishi.

**Mpango Mkakati wa Kudhibiti VVU na UKIMWI wa Sekta ya Afya wa mwaka 2017-2022**: Mkakati huu unazingatia matumizi ya kondomu kama afua muhimu ya kiafya katika kudhibiti VVU na maambukizi kupitia ngono. Mpango Mkakati huu unaunga mkono Mkakati wa Kondomu katika kuimarisha utoaji, ubora, uhamasishaji na usambazaji wa kondomu Nchini.

**Mpango Uendeshaji wa Kudhibiti VVU na UKIMWI wa Taifa wa mwaka 2016-2018**: Mpango huu uliunga mkono Mkakati wa Tatu wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI ambao ulilenga kutoa miongozo inayohusu mbinu jumuishi za kudhibiti VVU/UKIMWI ili kupunguza kabisa maambukizi mapya. Vilevile, mpango ulilenga kuzipa kipaumbele Afua pamoja na jitihada, ili kufikia malengo ya 90-90-90 ya kudhibiti na kutoa tiba ya UKIMWI ifikapo mwaka 2020, sambamba na Mkakati wa Mpango wa dharura wa Umoja wa Mataifa wa Kudhibiti na kutokomeza UKIMWI ifikapo mwaka 2030.

**Mpango wa Taifa wa Utekelezaji wa Uzazi wa Mpango Uliohuishwa** wa **mwaka 2019-2023:** Lengo la Mpango wa Taifa wa Utekelezaji wa Uzazi wa Mpango uliohuishwa ni kuwawezesha wanawake, vijana na wanandoa Nchini Tanzania kufikia utashi wao wa kuwa na watoto kwa kuhakikisha upatikanaji wa huduma nzuri na zenye viwango vya juu, pamoja na taarifa sahihi. Kwa kufanya hivyo, kiwango cha matumizi ya njia za kisasa za uzazi wa mpango Tanzania miongoni mwa wanawake wenye ndoa kinakadiriwa kuongezeka kutoka asilimia 36 kwa mwaka 2019 hadi asilimia 47 kwa mwaka 2023, na miongoni mwa wanawake wote inakadiriwa kuongezeka kutoka asilimia 30 kwa mwaka 2019 hadi asilimia 40 ifikapo mwa 2023.

### 1.2.1 Mkakati wa Kondomu

Mwaka 2015, Serikali kupitia Mkakati wa Kudhibiti UKIMWI ulitayarisha Mkakati wa kwanza wa Kondomu wa Taifa uliozinduliwa mwaka 2016 na kuungwa mkono na Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Marekani Mkakati huo uliodumu kwa miaka miwili ulilenga kushughulikia vipaumbele vya kimkakati vinavyolenga kupunguza maambukizi ya VVU, maambukizi kupitia ngono, pamoja na mimba zisizotarajiwa.

Vilevile, Mkakati ulitumia mfumo wa masoko jumuishi unaohusiana na programu za kondomu, ambapo Serikali ya Tanzania iliratibu soko lote la kondomu. Mkakati huu kupitia mfumo jumuishi wa Taifa ulilenga katika kuimarisha maeneo manne muhimu ambayo ni:

Uboreshwaji wa uongozi na uratibu, Usalama wa Usambazaji wa bidhaa, Uhitaji, na Mfumo wa msaada.

Kwa sasa Tanzania inatekeleza Mkakati wanne wa Taifa wa Kudhibiti VVU na UKIMWI kwa mwaka 2019-2023, ambao unasisitiza matumizi ya kondomu kama sehemu ya kudhibiti VVU na UKIMWI kupitia mfumo wa masoko jumuishi. Malengo makuu ya Mkakati ni kuongeza kiwango cha matumizi ya kondomu, pamoja na masuala mengine yanayohusu kondomu miongoni mwa jamii kwa ujumla na makundi maalumu yaliyo katika uhatarishi. Viashiria vya mkakati huu vimeorodheshwa hapa chini:

**Mfumo wa Jumuishi wa Kuratibu Programu za Kondomu katika Mkakati wa Nne wa Kudhibiti VVU na UKIMWI:**

i. Watu wazima (15-49): Matumizi ya kondomu yaliyo ripotiwa wakati wa kujamiiana kwa mara ya mwisho kwa watu wazima wenye wenza wengi yameongezeka kutoka asilimia 35 kwa wanaume na asilimia 27.78 kwa wanawake ikiwa ni wastani wa takwimu zilizoripotiwa kwa mwaka 2017 hadi asilimia 50 kwa mwaka 2020 na asilimia 95 ifikapo mwaka 2023.

ii. Vijana (15-24): Matumizi ya kondomu yaliyo ripotiwa wakati wa kujamiiana kwa mara ya mwisho kwa vijana wenye umri kati ya miaka 15-24 yameongezeka kwa asilimia 42 kwa wanaume na asilimia 37 kwa wanawake, ikiwa ni wastani wa takwimu zilizotolewa mwaka 2016 hadi asilimia 60 kwa mwaka 2020, na asilimia 80 ifikapo mwaka 2023.

iii. Makundi Maalumu: Matumizi ya Kondomu yaliyoripotiwa kwa kujamiiana kwa mara ya mwisho kwa makundi yaliyo katika hatari zaidi (SW) kuwa na wapenzi wao wa hivi karibuni yameongezeka kutoka asilimia 32 ya wastani wa takwimu zilizoripotiwa mwaka 2013 hadi asilimia 80 kwa mwaka 2020 na asilimia 100 ifikapo mwaka 2023.

Mikakati ya Mpango huu katika kufikia haya malengo ni pamoja na:

- Kuongeza kiwango cha usambazaji wa kondomu kwenye sekta za umma kwa kutumia majukwaa ya kijamii, sehemu za kazi, na maeneo mengine muhimu.
- Kuboresha utoaji, ubora, ununuzi na usambazaji wa kondomu katika ngazi zote, hasa katika ngazi ya jamii.
- Kuimarisha mfumo wa Tathmini na Ufuatiliaji wa programu za kondomu ili kuwepo na taarifa sahihi zinazohusu programu za kondomu

- Kuimarisha majukumu ya sekta za umma, masoko ya kijamii, makampuni ya kijamii, na sekta za biashara, ili kuyafanya yawe sawia na imara
- Kushughulikia unyanyapaa na ubaguzi unaohusiana na upataji wa kondomu miongoni mwa vijana, hasa wasichana balehe na vijana balehe.

Ili mpango wa kondomu ufikie malengo ya Mkakati wa Nne wa Taifa wa Kudhibiti VVU na UKIMWI, usambazaji wa kondomu ulipaswa kuongezeka kutoka kondomu milioni 248 kwa mwaka 2018 hadi kufikia kondomu 262 kwa mwaka 2020. Matarajio ni kwamba idadi ya wanaume itaongezeka kwa asilimia 20.8 kwa kila mwaka kati mwaka 2021-2023.

Mpango Mkakati wa Utekelezaji wa Uzazi wa Mpango ni kukuza huduma za Afya na Uzazi. Mpango shirikishi wa utekelezaji wa mwaka 2010-2015 unalenga kuongeza kiwango cha matumizi ya njia za kuzuia mimba kwa kuongeza kiwango cha upatikanaji na matumizi ya kondomu kama njia mojawapo ya uzazi wa mpango. Kulingana na Utafiti wa Afya na Demografia wa mwaka 2015/2016, matumizi ya kondomu kama njia ya uzazi wa mpango yalikuwa ni asilimia 3.9 miongoni mwa wanandoa wapya na wanawake wasioolewa wenye umri kati ya miaka 15-49. Kondomu za kiume na sindano ni njia za uzazi wa mpango zinazotumika kwa asilimia 15 kwa kila moja. Hata Hivyo, takwimu kutoka katika ripoti ya uchambuzi wa taarifa zinaonyesha kwamba kuna matarajio ya kuongezeka kwa kiwango cha matumizi ya kondomu kama njia ya uzazi wa mpango kwa asilimia 9 kwa mwaka 2019 na 2020[3]. Vilevile makisio yanaonyesha kwamba kondomu milioni 23.6 na milioni 26.7 zinanunuliwa na kusambazwa kwa ajili ya uzazi wa mpango kwa mwaka 2019 na 2020.

### 1.3 Dhana ya Mfumo wa Masoko Jumuishi ya Kondomu

Dhana ya masoko jumuishi ni mfumo ambao unaweza kutumika katika kutayarisha mikakati inayolenga kuongeza upatikanaji wa bidhaa za afya muhimu katika namna ya usawa na stahiki. Mfumo wa Masoko Jumuishi unalenga kuongeza ufanisi, usawa, uthibiti wa masoko kupitia uratibishwaji sekta ya umma, masoko, jamii, na biashara.

Mkakati wa Mfumo wa Masoko Jumuishi utasaidia kupunguza vizuizi katika matumizi ya kondomu kupitia afua stahiki na mtambuka. Ni muhimu sana kutambua nguvu ya bei na sehemu (yanashughulikiwa kupitia usambazaji wa kondomu) dhidi ya sababu zingine (yanashughulikiwa vizuri zaidi kupitia Mawasiliano ya mabadiliko ya Tabia katika Jamii na uhamasishaji wa kondomu. Usambazaji wa kondomu za bure au zenye punguzo kupitia vituo vya afya, maduka madogo madogo, au asasi za kijamii, ni suluhu sahihi ya uongezaji wa

[3] Quantification of Reproductive, Maternal, Newborn and Child Health Commodities for Mainland Tanzania, Forecasts for the period January 2019 to December 2020

upatikanaji wa kondomu katika maeneo magumu kufikika au maeneo duni. Ikiwa kondomu za bure na zenye punguzo zitaendelea kutiliwa mkazo zitahatarisha majina/chapa ya sekta ya biashara ambayo yanahitajika sana kwenye maduka ya dawa na majukwaa mengine ya kibiashara mijini.

Mfumo wa Masoko Jumushi unapendekeza kwamba kama tafiti za demografia pamoja na zinginezo zitabainisha sababu zinginezo za watu kutotumia kondomu (kama vile kutokuwa na mwitikio wa uhitaji wa matumizi ya kondomu, aibu, au mpenzi kukataa), basi mbinu sahihi zaidi ni kuongeza uhitaji kwenye nyanja ya majadiliano ya mabadiliko ya tabia katika jamii, hii itasaidia kuongezeka kwa kiwango cha matumizi ya kondomu. Ikiwa vipengele vyote vya uhitaji na usambazaji vipo, basi Mkakati wa Mfumo wa Masoko Jumuishi unapaswa kupambanua/kuweka bayana majukumu/kazi stahiki za sekta mbalimbali katika kuongeza uhitaji na usambazaji wa kondomu.

Katika miaka ya hivi karibuni, kumekuwa na mabadiliko ya haraka katika sekta ya afya na uchumi nchini Tanzania.Wakati serikali ya Tanzania inajikita katika kutokomeza kabisa maambukizi ya VVU pamoja na kulenga kufikia malengo ya dunia ya 90-90-90 ifikapo mwaka 2020, inapaswa kuhakikisha uwepo wa mkakati sahihi ya upatikanaji wa rasilimali za kutosha ili kuwafikia watu duni na makundi yaliyo katika mazingira hatarishi. Ili kupanua wigo wa haya mabadiliko na kuhakikisha uwepo wa soko lenye ubora linalokidhi mahitaji ya afya ya umma/wananchi katika namna ya ufanisi, ubora na endelevu, Mkakati wa kuteka soko lote la kondomu unahitajika.

Mkakati huu unatekeleza programu ya Mfumo wa Masoko Jumuishi, ambapo Serikali ya Tanzania kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto (Mpango wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI na Huduma za Afya ya Uzazi na Mtoto kwa kuratibu soko lote la kondomu. Sekta zingine pia zinachangia katika ufanikishwaji wa Mkakati wa Serikali. Vilevile kuna taratibu na sera zinazoweza kufanikisha utekelezwaji wa programu za kondomu kwa lengo la kuongeza matumizi ya kondomu sahihi na endelevu.

### 1.4 Mchakato wa utayarishaji wa Mkakati wa Kondomu

Lengo la utayarishaji wa Mkakati huu lilikuja kufuatia Mkakati wa kwanza wa Taifa wa Kondomu wa mwaka 2016-2018 kupitwa na wakati, sambamba na kuunganisha na Mikakati wa Taifa ya Kudhibiti VVU na UKIMWI kama vile: Mkakati wa Nne wa Taifa wa Kudhibiti VVU na UKIMWI (2018/19-2022/23), Mpango Mkakati wa nne wa Kudhibiti VVU na UKIMWI wa Sekta ya Afya, na Utafiti wa Viashiria na Matokeo ya VVU na UKIMWI

Tanzania wa mwaka 2016-2017. Mchakato ulihusisha kufanya uchambuzi wa kina pamoja na tathimini ya changamoto na vipaumbele vilivyokwisha kubainishwa kwenye Mkakati Uliomalizika muda wake. Katika hatua hii, Wadau muhimu kutoka sekta za Kiserikali, Wadau wa Maendeleo, Asasi za masoko na kampuni za kijamii, sekta za biashara na zinginezo zimeshirikishwa katika mchakato.

Lengo kuu la utayarishaji wa Mkakati ni kushughulikia mafanikio na changamoto zilizobainishwa wakati wa utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Kondomu wa mwaka 2016-2018, ili kuandaa Mchakato wa miaka mitano wa Taifa wa Kondomu kwa kipindi cha kati ya mwaka 2019-2023. Hivyo, mtaalamu mshauri alifanya uchambuzi wa taarifa na takwimu zinazohusiana na Sera na mipango ya kondomu. Vilevile alifanya mahojiano na wadau 45 muhimu, ambao ni wawakilishi kutoka Wizara, Idara Zinazojitegemea na Wakala za Serikali, Wabia wa Maendeleo, Sekta binafsi Taasisi na Asasi za kiraia. Matokeo ya kina ya Utafiti yamejumuishwa kwenye Mkakati, hivyo kuwa kama kigezo cha uboreshwaji wa Mkakati huu na kuwa na matokeo tofauti tofauti ambayo yaligawiwa na kuboreshwa wakati wa vikao vya ushauri na tathimini.

## SEHEMU YA 2: UCHAMBUZI

### 2.1 Matokeo ya mapitio ya nyaraka na vikao vya ushauri vya uchambuzi wa taarifa na takwimu.

#### 2.1.1 Matumizi ya Kondomu Nchini Tanzania

Kondomu bado inazingatiwa kama bidhaa pekee yenye uwezo wa kutoa kinga za aina tatu kwa pamoja ambazo ni kinga dhidi ya maambukizi ya VVU, mambukizo kupitia ngono pamoja na mimba zisizotarajiwa.[4] Uthibitisho kutoka tafiti za kisayansi unaonyesha kuwa kondomu ya kiume aina ya Latex inakinga maambukizi ya VVU na maambukizo kupitia ngono kwa ufasaha kwa zaidi ya asilimia 80.[5] Kumekuwa na mafanikio ya muda mefu na endelevu ya matumizi ya kondomu nchini Tanzania, tangu uanzishwaji wa matumizi ya kondomu kama njia ya uzazi wa mpango miaka ya 1970 na baadae kufanywa kuwa kinga dhidi ya maambukizo kupitia ngono mnamo mwaka 1987.

##### 2.1.1.1 Matumizi ya kondomu kama njia ya kuzuia mimba

Mpango wa Utekelezaji wa Uzazi wa Mpango Uliothaminishwa wa mwaka 2010-2015 unatambua na kusisitiza umuhimu wa matumizi ya kondomu kwa usalama thabiti. Mpango wa Utekelezaji wa Uzazi wa Mpango Uliothaminishwa wa mwaka 2010-2015 ulilenga kuziongoza programu za Uzazi wa Mpango ili kuongeza kiwango cha matumizi ya njia za kisasa za uzazi wa mpango miongoni mwa wanawake walio katika umri wa kuzaa kutoka asilimia 28 kwa mwaka 2010 hadi asilimia 60 kwa mwaka 2015. Hata hivyo, wakati wa utekelezaji, Kiwango cha matumizi ya njia za Kisasa za uzazi wa mpango (mCPR) kiliongezeka kutoka asilimia 27 hadi asilimia 32[6]. Idadi kubwa ya wanawake wanaotumia njia za uzazi wa mpango wanatumia njia za kisasa za uzazi wa mpango (Asilimia 32 ya wanandoa wa hivi karibuni wanatumia njia za kisasa za mpango wa uzazi). Ni asilimia mbili tu (2%) ya wanawake walioolewa imetaarifiwa wanatumia kondomu. Kuna kiwango kikubwa cha matumizi ya njia za uzazi wa mpango miongoni mwa wanawake wasioolewa wanaoshiriki ngono kinachosababishwa na matumizi ya kondomu pamoja na sindano. Takwimu zinaonyesha kuwa asilimia ya wanawake wasioolewa wanaoshiriki ngono na wenye umri wa kati ya miaka 15-49, asilimia 54 wanatumia njia zingine za uzazi wa mpango, na asilimia 46 wanatumia njia za kisasa. Hii inadhihirisha kuwa kiwango cha matumizi ya kondomu na sindano ni njia za uzazi wa mpango zinazotumiwa zaidi kwa asilimia 15 kwa kila moja.[7]

---

[4] UNAIDS: Strengthening Condom Programmes and Markets in Africa; 2019
[5] http://www.who.int/hiv/topics/condoms/en/
[6] NFPCIP 2019-2023
[7] TDHS 2015-2016

Kuhusu Uelewa wa pamoja juu ya njia za uzazi wa mpango nchini Tanzania, asilimia 99 ya wanawake walioolewa hivi karibuni wenye umri wa kati ya miaka 15-49 na asilimia 100 ya wanaume waliooa hivi karibuni wenye umri wa kati ya miaka 15-49 wanaelewa angalau njia mojawapo ya uzazi wa mpango. Vilevile, Uelewa juu ya matumizi ya kondomu ya kiume kama njia ya uzazi wa mpango ni karibu sawa kwa kila mwanamke na mwanaume, wakati uelewa kuhusu kondomu za kike ni asilimia 70.

**Jedwali la 1: Uelewa juu ya matumizi ya Kondomu kama njia ya uzazi wa mpango.**

| Uelewa juu ya Kondomu kama njia ya uzazi wa mpango | Wanawake wote | Wanawake walioolewa | Wanawake wasioolewa wanaoshiriki ngono | Wanaume wote | Wanaume waliooa | Wanaume wasiooa wanaoshiriki ngono |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Kondomu za kiume** | 94.8% | 95.8% | 98.9% | 96.2% | 98.5% | 97.9% |
| **Kondomu za kike** | 79.7% | 80.8% | 89.2% | 79.7% | 86.7% | 81.8% |

**Chanzo:** TDHS 2015-2016

### 2.1.1.2 Matumizi ya kondomu kama njia ya kujikinga na maambukizi ya VVU na Maambukizo kupitia Ngono

Matumizi sahihi na endelevu ya kondomu ya kiume aina ya latex yanapunguza hatari ya kupata maambukizi ya VVU na maambukizo kupitia ngono. Kuongeza kiwango cha upatikanaji, ufikiwaji, na uwezo wa kumudu gharama za kununua kondomu za kike na kiume miongoni mwa jamii na makundi maalumu kwa njia ya programu lengwa za usambazaji ni kipengele muhimu katika mwitikio wa VVU. Takwimu za sasa zinaonyesha matumizi ya kondomu wakati wa kujamiiana kwa mara ya mwisho miongoni mwa makundi ya kawaida Tanzania Bara ni chini ya asilimia 60. Vilevile takwimu zinaonyesha kuwa kiwango cha matumizi ya kondomu wakati wa kujamiiana kwa mara ya mwisho kimeshuka kutoka asilimia 58 kwa wanawake, na asilimia 59 kwa wanaume kwa mwaka 2012 hadi asilimia 27.3 kwa wanawake na asilimia 34.9 kwa wanaume kwa mwaka 2016[8]. Pia, kiwango cha matumizi ya kondomu wakati wa kujamiiana kwa mara ya mwisho miongoni mwa wanawake waishio vijijini kiko chini kwa asilimia 37.6 ikilinganishwa na asilimia 48.8 ya wanawake waishio mjini.

[8] THIS 2016-2017

Bado kuna ufinyu wa ufikiwaji wa kondomu, hasa miongoni mwa vijana balehe na vijana, kwa sababu ya unyanyapaa unaohusishwa na ulizaji au ununuaji wa kondomu, gharama, kuisha/kumalizika kwa kondomu, pamoja na kiwango hafifu cha masoko na usambazaji. Miongoni mwa vijana, ni asilimia 37 ya wanawake na asilimia 41 ya wanaume tu ndiyo iliyoripotiwa kutumia kondomu wakati wa kujamiiana kwa mara ya mwisho. Wasichana na wanawake waliripotiwa kutokuwa na uelewa wa kutosha wa kujadiliana juu ya matumizi sahihi ya kondomu wakati wa kujamiiana kutokana na kukosekana kwa usawa wa kijinsia, pamoja na mitazamo ya kimila. Kiwango cha matumizi ya kondomu wakati wa kujamiiana kwa mara ya mwisho na wapenzi wasio na ndoa na wasioishi pamoja ni asilimia 36 kwa wanawake na asilimia 30 kwa wanaume.[9]

Kiwango cha matumizi ya kondomu kimeripotiwa pia kuwa chini miongoni mwa makundi maalumu. Asilimia 89 ya wanaume na asilimia 75 ya wanawake walio miongoni mwa wajidunga na wenye wenza wasiojidunga wameripotiwa kutokuwa na matumizi endelevu ya kondomu wakati wa kujamiiana na wapenzi wao wa mara kwa mara (matumizi hatarishi miongoni mwa watu wanaojidunga dawa za kulevya Temeke kwa mwaka 2011). Miongoni mwa Wanawake wanaofanya biashara ya ngono, asilimia 69.3 waliripoti kuwa na matumizi endelevu ya kondomu wanapojamiiana na wateja wao wa mara kwa mara, ingawa ni asilimia 31.6 tu ya wanawake wanaofanya biashara ya ngono wameripotiwa kuwa na matumizi endelevu ya kondomu wanapojamiiana na wateja walewale kwa kipindi cha siku 30. Pia, Asilimia 43.2 ya wanaume wanaofanya ngono na wanaume wenzao hawakutumia kondomu walipojamiiana kwa mara ya mwisho na wapenzi wao wasio rasmi, wakati asilimia 49.1 walitumia kondomu walipojamiiana kwa mara ya mwisho na wapenzi wao wa mara kwa mara. Aidha, takribani asilimia 30 ya wahojiwa wote waliripotiwa kujihusisha na biashara ya ngono (Matumizi ya Kondomu kwa wanaume wanaofanya ngono na wanaume wenzao, mwaka 2013).

### 2.2 Ulinganifu waTanzania Katika Nchi za Mashariki na Kusini mwa Afrika

Upatikanaji wa kondomu unatofautiana kwa kila Nchi, ambapo ni Nchi tano tu zilifikia lengo la Mfuko wa Umoja wa Mataifa wa Idadi ya Watu la ulinganifu wa kimkoa wa ugawaji wa kondomu za kiume 30 kwa kila mwanaume na kwa kila mwaka, kati ya mwaka 2011 na mwaka 2014. Matumizi ya kondom yaliyo ripotiwa wakati wa kujamiiana kwa mara ya mwisho kwa watu wazima wenye wapenzi wengi kwa kipindi cha miezi 12 iliyopita kinakadiriwa kuwa chini kwa asilimia 23 miongoni mwa wanaume na asilimia 33 miongoni mwa wanawake. Vilevile, kuna tofauti kubwa ya kiwango cha matumizi ya kondomu

[9] NMSF 2018/2019-2022/2023

miongoni mwa nchi, ambapo inakadiriwa kuwa kati ya asilimia 7 miongoni mwa wanaume wanaoishi Madagaska hadi asilimia 83 miongoni mwa wanaume wanaoishi Swatini. Sambamba ya hayo, Kiwango cha matumizi ya kondomu kimeripotiwa kuwa juu kwa asilimia 60 kwa wanaume wanaoshiriki ngono ya kulipia.

Matumizi ya kondomu yaliyo ripotiwa wakati wa kujamiiana kwa mara ya mwisho na mtu yeyote mwenye umri kati ya miaka 15-49 Nchini Tanzania, yanakadiriwa kuwa asilimia 24 kwa wanaume na asilimia 13 kwa wanawake yakilinganishwa na Namibia ambapo asilimia 57 ni wanaume na asilimia 41 ni wanawake. Hata hivyo Tanzania inashika nafasi ya pili dhidi ya Kenya katika utumiaji wa kondomu za kiume ndani ya Jumuiya ya Africa Mashariki.

Tanzania inaripotiwa kuwa na kiwango cha juu cha asilimia ya wanawake wanaotumia kondomu wakati wakujamiiana katika ngono ya mwisho na mtu yeyote. Kwa ujumla nchi za Afrika Mashariki zinaripotiwa kuwa na matumizi hafifu ya kondomu wakati wa kujamiiana na mtu yeyote ikilinganishwa na Nchi za Kusini mwa Afrika. Ingawa nchi ya Afrika Kusini iliripotiwa kuwa na kiwango kikubwa cha usambazaji wa kondomu, Tanzania ilikuwa ya pili dhidi ya Kenya katika usambazaji wa kondomu kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki. Hata hivyo, katika Jumuiya ya Afrika Mashariki Kenya na Uganda zimesambaza zaidi kondomu za kike. Pamoja na jitihada zinazoendelea za usambazaji wa kondomu, Tanzania imebaki kuwa miongoni mwa Nchi sita ambazo hazijafikia lengo la kusambaza kondomu kwa mtu mmoja mmoja. Nchi zingine ni pamoja na Malawi, Mzumbiji, Swatin, Zambia na Uganda.

### 2.3 Uchambuzi wa Masoko

Ingawa soko la kondomu linazidi kushamiri, zipo changamoto na fursa zimebainiwa kulikabili soko la kondomu. Soko la kondomu linajumuisha ukubwa (idadi ya kondomu) na kina (aina za kondomu), pamoja na wadau/wahusika walio kwenye mifumo ya usambazaji. Vikwazo vya uzalishaji katika ngazi yoyote vinaweza kuathiri kiwango cha matumizi ya kondomu, bila kujali kama ni sekta ya umma, sekta binafsi, masoko ya kijamii, au sekta za biashara za kondomu. Vipengele hivi vinaweza kugawanywa kama ifuatavyo:

#### 2.3.1 Wadau/wahusika katika soko la kondomu

Wakati kukiwa bado kuna uhitaji mkubwa katika afya ya jamii kuhusu kuhamasisha na kuongeza kiwango cha matumizi ya kondomu kwa ajili ya uzazi wa mpango, pamoja na kudhibiti maambukizi ya VVU na magonjwa ya ngono, Wadau wa Maendeleo wanaendelea kujadiliana juu ya matumizi sahihi ya punguzo kwa jamii, pamoja na kazi ya wadau/wahusika

wasio wa kiserikali katika ununuzi, uhamasishaji, na usambazaji wa kondomu[10]. Mbali na kazi za mifumo ya usambazaji, Uongozaji na uratibu wa Kiserikali ni muhimu katika kushughulikia programu za kondomu. Hizi ni pamoja na sera na udhibiti, ubora, na kazi za kitaifa za makadirio, utoaji wa fedha na uhamasishaji. Kufuatia uchambuzi wa kutosha na wa kina wa soko la kondomu Tanzania, pamoja na tathimini katika vituo vya afya, zifuatazo ni changamoto na fursa zilizobainiwa.

#### 2.3.1.1 Mahitaji ya kondomu ikilinganishwa na uhitaji na ugavi

Tanzania inaripotiwa kuwa miongoni mwa nchi 12 zenye maambukizi ya juu ya VVU, ambapo zaidi ya asilimia 40 ya wanaume watu wazima wenye umri wa kati ya miaka 15-64 wanashiriki ngono isiyo rasmi. Uwiano/wastani katika usambazaji wa kondomu katika nchi mbalimbali ambapo zaidi ya asilimia 40 ya wanaume watu wazima wanaoshiriki ngono isiyo rasmi ni kondomu 40 kwa kila mji. Hata hivyo Usambazaji wa kondomu kwa Tanzania umebaki kuwa kondomu 13 tu kwa kila mji[11].

Mwaka 2014, kulifanyika mapitio ya jumla ya uhitaji wa kondomu, mapitio ya jumla ya uhitaji wa kondomu ni makisio ya kiasi cha bidhaa kinachohitajika ili kufikia lengo la ufikiaji/ueneaji wa kondomu kwa wote kila mwaka, usambazaji huru na hali ya sasa ya ufikiaji/ueneaji. Ukokotoaji wa uhitaji wa kondomu kwa wote katika kujikinga dhidi ya maambukizi ya VVU yanategemea idadi ya matendo ya ngono hatarishi kwa mwaka, na kwa makisio kwamba kondomu moja inakinga tendo moja la ngono. Matendo ya ngono hatarishi ni makisio ya nchi yanayojumuisha: biashara ya ngono, ngono na mpenzi wa nje ya ndoa, na ngono ya wanandoa ambapo mwenzi mmojawapo ana mpenzi nje ya ndoa. Kulingana na takwimu za Utafiti wa Demografia na Afya, pamoja na sensa, inakadiriwa kuwa uhitaji wa kondomu kwa mwaka nchini Tanzania ni takribani kondomu milioni 260[12].

Katika Mkakati wa Kondomu wa mwaka 2016-2018, usambazaji wa kondomu ulikisiwa kukidhi asilimia 40-50 ya lengo la uhitaji wa kondomu kwa wote. Hata hivyo, uwepo wa uhitaji wa kondomu kwa wote, hauna maana ya kuwianisha ufasaha wa uhitaji wa kondomu, na hiki kinakuwa ni kigezo cha uhitaji na ueneaji wa kondomu wa sasa unaotarajiwa kutoka kwenye uwekezaji wa Mawasiliano ya mabadiliko ya tabia katika jamii na uhamasishaji wa matumizi ya kondomu. Wakati ambapo inaweza kuchukua miaka kadhaa katika kufika lengo la uhitaji wa kondomu kwa wote katika nchi mahususi, ongezeko la watu katika matumizi ya kondomu linaweza kutumika katika makadirio ya

[10] USAID; Using Total Market Approaches in Condom Programs,2015
[11] GARPR2012 (UNKNOWN)
[12] HIV Dodoma

mahitaji ya kiwango cha juu cha kondomu. Kwa mfano, makisio ya ongezeko la asilimia 20 katika uhitaji wa kondomu ni idadi itakayotumika kwenye makadirio ya mahitaji ya usambazaji wa kondomu.

#### 2.3.1.2 Uhitaji/matumizi ya kondomu

Matumizi ya kondomu yanaweza kutumika katika makadirio ya uhitaji wa kondomu. Utafiti wa Demografia na Afya Tanzania umeonesha kuwa, kwa kipindi cha miezi 12 iliyopita asilimia 23.6 ya wanaume wameripotiwa kutumia kondomu wakati wa kujamiiana kwa mara ya mwisho, wakati matokeo ya mwaka 2014 yanabainisha kuwa asilimia 27.2-31.3 ya wanaume walitumia kondomu wakati wa kujamiiana kwa mara ya mwisho. Utafiti wa viashiria vya VVU na UKIMWI Tanzania wa mwaka 2016-2017, uliofanya utafiti juu ya wa watu wasio na ndoa, na wapenzi wasioishi pamoja umebainisha kuwa, asilimia 31.7 ya watu wazima wenye umri wa zaidi ya miaka 15 wameripotiwa kutumia kondomu wakati wa kujamiiana kwa mara ya mwisho, ambapo asilimia 34.9 ni wanaume, na asilimia 27.3 ni wanawake[13]. Hata hivyo mbinu za uchambuzi zinatofautiana, hivyo matokeo ya utafiti yanapaswa kufasiriwa kwa umakini. Licha ya hivyo, wakati kiwango cha matumizi ya kondomu kinazidi kukua miongoni mwa makundi rika, bado kuna nafasi ya kuboresha kiwango cha matumizi ya kondomu.

**Jedwali la 2: Kiwango cha matumizi ya kondomu miongoni mwa makundi rika mbalimbali.**


| Population Segment | 2010 TDHS* | 2011-2012 THMIS* | 2016-2017 THIS |
|---|---|---|---|
| **Wanaume wa mijini (15-49)** | 32.0 | 43.8 | 48.8 |
| **Wanaume wa vijijini (15-49)** | 21.5 | 22.2 | 37.6 |
| **Wanaume (20-24 yrs)** | - | 38.8 | 39.8 |
| **Wanaume, Vijana (15-24)** | 36.2 | 40.6 | 33.5 |
| **Wanaume, Vijana (15-19)** | 34.2 (hawajawahi kuoa, 46.1) | - | 24.2 |
| **Wanawake, Vijana (15-19)** | 35.3 (hawajawahi kuolewa, 50.2) | - | 29.2 |

[13] THIS 2016 - 2017

### 2.3.2 Usambazaji endelevu wa kondomu

Kwa kuzingatia sekta zinazohusiana na masuala ya kondomu kama vile sekta ya umma, ya masoko ya kijamii, ya makampuni ya kijamii na ya biashara ya kondomu, inakadiriwa kuwa usambazaji wa kondomu unakidhi takribani asilimia 40-50 ya uhitaji wa kondomu.[14] Takwimu zilizotolewa na wadau wa usambazaji wa kondomu zinadai kwamba wakati soko la kondomu linakidhi lengo la asilimia 40-50 la uhitaji wa kondomu, bado kuna kushuka kwa kiwango cha kondomu zinazosambazwa kwa kipindi cha muda mrefu, kutoka mwaka 2016 hadi mwaka 2019. Sababu ya kushuka kwa Kiwango cha usambazaji imeripotiwa kuwa ni kutokuwepo kwa fedha za kutosha kusaidia usambazaji wa kondomu katika sekta binafsi pamoja na masoko ya kijamii.

**Kielelezo cha 1: Kiasi cha Usambazaji wa Chapa/aina za Kondomu**





[14] Supply estimates for public sector are taken from MSD distribution records. Social marketing sector is taken from PSI and T-MARC program records. More so, the 2019 data for Zana/Cupid Condom records from MSD was extracted from 1st July 2018 to 3rd July 2019

### 2.3.3 Upana wa/ Kina cha Soko

Kiwango cha Usambazaji wa kondomu nchini Tanzania kiliendelea kuongezeka hadi kufikia mwaka 2016/2017 ambapo Usalama wa usambazaji wa bidhaa pamoja na masuala ya fedha kwenye sekta ya masoko ya kijamii kilisababisha kuporomoka kwa soko la kondomu.[15] Kiwango cha gawio la kondomu katika sekta ya masoko ya kijamii, kama vile asilimia ya kondomu zote zilizosambazwa kimeongezeka pia. Vilevile, kumekuwa na ongezeko kiasi kwenye mauzo katika sekta ya biashara na wakati huohuo kuporomoka kwa kiwango cha gawio la kondomu zinazosambazwa kwenye sekta ya umma

[15] Mann Global Health: Tanzania Case study

**Kielelezo cha 2: Kondomu zilizosambazwa na Wadau wa masoko**




**Chanzo:** Mann Global Health - Tanzania Case study, 2018

### 2.4 Vikwazo/vizuizi katika matumizi ya kondomu

Pamoja na kwamba sasa kuna uelewa wa kutosha juu ya matumizi ya kondomu, bado kuna uwepo wa vikwazo mbalimbali. Hivi vikwazo vinapaswa kushughulikiwa ili kuendeleza hali ya uhitaji na ongezeko la matumizi ya kondomu.

Vikwazo hivyo vimegawanyika katika sehemu kuu nne:

#### 2.4.1 Fursa katika ufikiaji wa kondomu

Hizi zinajumuisha vikwazo vya gharama na ufikiaji. Wakati utafiti uliofanywa kuhusu utayari wa kulipia gharama za kondomu unabainisha kuwa wanaume wana utayari zaidi wa kununua kondomu, baadhi ya makundi lengwa hasa wanaume maskini na wale wa vijijini wanaendelea kukabiliwa na changamoto ya ufikiaji, pamoja na gharama ya kumudu manunuzi ya kondomu. Licha ya zaidi ya asilimia 80[16] ya vijiji/mitaa iliyofanyiwa utafiti nchini Tanzania kuwa na angalau sehemu moja ambapo kondomu zinaweza kununuliwa, asilimia 44[17] ya watu wangeweza kutumia kondomu zaidi iwapo zingepatikana kwa urahisi.

#### 2.4.2 Uelewa/uwezo wa kutumia au kujadiliana kuhusu matumizi ya kondomu

Kwa jumla, wanaume na wanawake wa rika zote wana elimu ya kutosha kuhusu matumizi ya kondomu kama kinga dhidi ya VVU[18]. Kwa kuwianisha makundi rika yote, asilimia 76.4% ya wanawake na asilimia 75.8 ya wanaume waliripotiwa kutumia kondomu kama kinga dhidi

[16] MAP FMCG 2014
[17] HIV Dodoma
[18] TDHS 2010

ya VVU. Hata hivyo, wanawake na wasichana wengi wanaendelea kukabiliwa na changamoto juu ya kujadiliana kuhusu matumizi ya kondomu kutokana na sababu za kimila, kutamaduni zinazoendeleza masuala ya kukosekana kwa usawa wa kijinsia. Asilimia 80.7% ya wanawake walijua mahali pa kuzipata kondomu ikilinganishwa na asilimia 88.1% ya wanaume.[19]

### 2.4.3 Upatikanaji wa kondomu

Tafiti mbalimbali zilizojikita kwenye maeneo yaliyoathirika zaidi na janga la VVU zimebainisha changamoto mbalimbali katika upatikanaji wa kondomu, changamoto hizi zimebainiwa pia katika maeneo yaliyo katika mazingira hatarishi zaidi ya kupata maambukizi ya VVU. Utafiti uliofanywa na Mpango wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI wa mwaka 2019 juu ya usambazaji wa kondomu ili kubaini upatikanaji wa aina/chapa na machaguo ya aina/chapa ya kondomu kwenye maeneo lengwa katika mikoa mitatu ya Tanzania Bara, umeonyesha kuwa aina tatu za kondomu zilitajwa kupendwa zaidi na makundi maalumu na yaliyoko katika mazingira hatarisha, kondomu hizi ni pamoja na Salama (asilimia 34.1), Dume (asilimia 23.1), na zana kondomu (13.3)[20]

**Jedwali la 3: Aina/chapa za kondomu zinazopendwa zaidi**

| Aina ya kondomu inayotumika sana | Namba | Asilimia |
|---|---|---|
| **Zana** | 53 | 13.3 |
| **Salama** | 136 | 34.1 |
| **Dume** | 93 | 23.3 |
| **Familia** | 21 | 5.3 |
| **Care** | 12 | 3.0 |
| **Lady Pep** | 13 | 3.3 |
| **Durex** | 16 | 4.0 |
| **Rough Rider** | 27 | 6.8 |
| **Bull** | 17 | 4.3 |
| **Lifeguard** | 11 | 2.8 |

**Chanzo:** NACP, 2019

[19] ibid.
[20] Gissenge L.I. Lija et al: Condom Distribution: Assessment of the Availability and accessibility in the Selected Hotspots of Dar es Salaam, Mwanza and Mbeya Cities, Tanzania

### 2.4.4 Mitazamo na Fikra/imani

Kikwazo kikubwa cha kimtazamo ni kukosekana kwa uelewa juu ya hatari, ambapo asilimia 50[21] ya watu wanadai kuwa hawahitaji kutumia kondomu ikiwa mahusiano yao ni ya uaminifu. Utafiti umeonyesha kuwa kiwango cha matumizi ya kondomu kimeshuka wakati wa kujamiiana na mpenzi wa kudumu/mara kwa mara. Vizuizi vingine katika matumizi ya kondomu ni pamoja na matumizi ya vileo/vilevi, pamoja na Imani za kidini na kiutamaduni. Kwa mfano, asilimia 38[22] ya watu wanaamini kwamba ngono/ kujamiiana ni jambo la siri na kwamba halipaswi kujadiliwa. Sambamba na hilo, asilimia 34[23] ya watu wanasikia aibu wanaponunua kondomu, hii ikijitokeza zaidi miongoni mwa vijana wenye umri mdogo.

## 2.5 Tofauti kuu za kijiografia katika upatikanaji wa kondomu

Kwa upande wa uelewa juu ya upatikanaji wa kondomu, asilimia 31 ya watumiaji wa kondomu wanakubali kuwa kondomu za kiume zinapatikana sana kwenye jamii pindi zinapohitajika, na asilimia 6 wanakubaliana kuwa kondomu za kike zinapatikana vilevile[24] Kiwango cha upatikanaji na ukubalikaji wa kondomu ni vikwazo vikuu kwa watumiaji katika sekta ya umma kwa asilimia 51.4 ikilinganishwa na watumiaji wa kondomu katika sekta ya masoko ya jamii ambayo ni asilimia 43.1, sambamba na hilo, kama ilivyoonyeshwa kwenye takwimu za kiasi cha kondomu kinachohitajika cha mwaka 2014, watumiaji wa kondomu kutoka sekta ya umma waliripotiwa kuwa na aibu katika kuchukua kondomu.

Utafiti wa kijiografia wa ueneaji na ufikiaji wa kondomu umedhihirisha kuwa, ufikiaji (asilimia ya watu wanaonunua bidhaa) wa kondomu kwenye mikoa 25 ya Tanzania iliyobainiwa ni wastani wa asilimia 43, ambapo kiwango katika mkoa wa Tanga kimeripotiwa kuwa chini kwa asilimia 22 na kiwango cha juu cha asilimia 63 katika mkoa wa Ruvuma[25], hii inadhihirisha tofauti kubwa ya kijiografia iliyopo katika upatikanaji wa bidhaa. Vilevile, asilimia 45 ya wale ambao hawakununua kondomu walidai kuwa bidhaa ya kondomu haina soko/hakuna wateja wa kutosha, hii inadhihirisha kuwa kuna kukosekana kwa uelewa wa mahitaji kunaongeza ufikiaji hafifu wa kondomu.

## 2.6 Uwepo wa sekta mahususi

Ingawa wale walio katika daraja la/hadhi ya juu ya kijamii na kiuchumi wanauwezekano mkubwa wa kununua na kutumia kondomu katika sekta ya biashara au zenye punguzo, matumizi ya kondomu kutoka sekta ya umma yapo kwenye kila daraja la kijamii na kiuchumi. Hii inadhihirisha kuwa wale wanaopaswa kumudu gharama za kununua kondomu

---
[21] Needscope 2013
[22] ibid.
[23] ibid.
[24] Omnibus 2014
[25] MAP FMCG 2014

kwenye masoko ya kijamii na sekta ya biashara wanafaidika na punguzo linalolenga kuwafikia walio kwenye daraja la chini la kijamii na kiuchumi.

### 2.7 Uelewa juu ya chapa/aina ya kondomu kulingana na mgawanyo wa Mfumo wa Masoko ya Jumuishi

Kondomu zenye punguzo kwenye masoko ya kijamii zinaripotiwa kutumika zaidi nchiniTanzania, ambapo Dume na Salama zimesemekana kutumika/kupendelewa zaidi. Hata hivyo matumizi na ukubalikaji wa kondomu kwenye sekta ya biashara unakua kwa kiwango kikubwa sana.[26] Hizi takwimu zinashabihiana na matokeo ya utafiti uliofanywa na Mpango wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI juu ya usambazaji wa kondomu ambao umebaini kuwa, kondomu zinazotumika/kupendwa zaidi ni Salama (asilimia 34.1), na Dume (asilimia 23.3) zikifuatiwa na kondomu za Zana (asilimia 13.3). Vilevile, utafiti ulionyeha kuwa fikra na mapendeleo ya aina kondomu kwa watumiaji wa kondomu ni kwamba, kondomu katika sekta ya masoko ya jamii ndizo zenye ubora wa juu, zimefungwa vizuri, za kuaminika na kufanya mtumiaji ajisikie vizuri/amani anapozitumia[27]. Karibu nusu ya wanaume nchini Tanzania wanaamini kuwa, aina /chapa ya kondomu ni lazima iwiane na mtumiaji/hadhi ya mtumiaji, ili kutoa fursa ya kunadi aina/chapa mbalimbali kwa taasisi muhimu.

### 2.8 Mafanikio na changamoto kuu katika uratibishaji wa programu za kondomu

#### 2.8.1 Uongozi na uratibu

| Kipengele | Mafanikio | Changamoto |
|---|---|---|
| Uratibu wa Wabia | - Kuwepo kwa kamati shirikisha za kondomu chini ya Kamati ya Kitaalamu ya kudhibiti VVU na UKIMWI zikiratibiwa na TACAIDS.<br>- Kuwepo kwa kamati za Usalama wa bidhaa za masuala ya afya ya uzazi zinazojumuisha suala la kondomu kwenye ajenda za vikao.<br>- Serikali kushughulikia uongozaji, uratibishaji na umiliki wa programu za kondomu. | -Kukosekana kwa ushirikishaji na uratibu wa kutosha wa afua za kondomu miongoni mwa wadau . |

[26] SHOPS PLUS 2019
[27] NACP,2019

| Kipengele | Mafanikio | Changamoto |
| --- | --- | --- |
| Uragibishi na utafutaji Rasilimali | - Uwepo wa Mkakati wa nne wa Kudhibiti UKIMWI wa mwaka 2018/19- 2022/23<br>- Uwepo wa Mkakati wa Taifa wa Kondomu.<br>- Suala la VVU zikiwemo programu za kondomu ni ajenda ya kudumu ya Wizara, Idara Zinazojitegemea na Wakala za Serikali<br>- Usimamizi mzuri wa sekta ya afya katika utunzaji wa rasilimali kwa ununuzi wa kondomu na ugawanyaji. | - Kukosekana viongozi mahiri wa kutosha wa kuhamasisha matumizi ya kondomu miongoni mwa viongozi wa kidini na kijamii.<br>- Kupungua kwa rasilimali za kutayarisha programu za kondomu<br>- Kukosekana kwa fedha za kutosha katika utekelezaji na ufuatiliaji. |
| Sera na Taratibu/ Kanuni | - Mazingira wezeshi ya sera kwa ajili ya ulinzi pamoja na nyaraka mahususi za sera zikiwemo:<br>o Mkakati wa nne wa Kudhibiti UKIMWI wa mwaka 2018/19 - 2022/23.<br>o Mpango Mkakati wa nne wa Kudhibiti UKIMWI wa Sekta ya Afya wa mwaka 2017- 2022.<br>o Muongozo wa Taifa wa usambazaji wa kondomu wa mwaka 2019<br>o Mpango wa Mpango wa Taifa wa Utekelezaji wa Uzazi wa Mpango liohuishwawa mwaka 2019 | - Usambazaji hafifu wa mkakati wa Taifa wa usambazaji wa kondomu wa mwaka 2016-18 pamoja na nyaraka zinazohusiana na masuala ya kondomu.<br>Ushirikiano usiotosha/dhaifu wa Sekta ya Umma na Binafsi |

| Kipengele | Mafanikio | Changamoto |
|---|---|---|
| | – 2023.<br>○ Waraka namba 2 na mwongozo wa kudhibiti VVU, UKIMWI na Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza (MSY) katika Utumishi wa Umma wa mwaka 2014. | |

**2.8.2** Uhitaji, upataji na utumiaji

| Kipengele | Mafanikio | Changamoto |
|---|---|---|
| Utafiti wa masoko | - Utafiti wa Mfumo wa Masoko Jumuishi uliofanywa na Mradi Kiongozi Katika Kuimarisha Ushiriki wa Sekta Binafsi katika Afya: ukiwemo utafiti wa ubora na wa ukaguzi wa manunuzi ya rejareja wa mwaka 2019.<br>- Shirika la Kimataifa Linalohudumia Jamii lilifanya utafiti wa mzunguko wa tatu na wa nne wa MAP juu ya ufikiaji wa soko la kondomu<br>- Shirika la Masoko na Mawasiliano, Shirika la Kimataifa linalohudumia Jamii, na asasi ya kimataifa ya kudhibiti VVU na UKIMWI, uzazi wa mpango na afya ya uzazi wamefanya utafiti wa | - Kiwango cha chini cha tafiti zinazohusu ueneaji wa upatikanaji wa kondomu<br>- Kukosekana kwa tafiti endeshaji zinazohusu kondomu za kike<br>- Usambazaji duni wa matokeo ya tafiti zinazohusu soko la kondomu kwa wadau.<br>- Kukosekana kwa tathmini ya mahitaji ya kondomu.<br>- Kukosekana kwa tafiti juu ya matumizi ya kondomu katika jamii za wafugaji, wachimbaji wa madini, wajenzi, wavuvi na kilimo na n.k.<br>- Kukosekana kwa tafiti juu ya matumizi ya kondomu kwa makundi maalumu na makundi hatarishi.<br>- Ufinyu wa elimu juu ya matumizi ya kondomu. |

| Kipengele | Mafanikio | Changamoto |
|---|---|---|
| | ufikiaji wa soko la kondomu.<br>- Utafiti wa bei wa Shirika la Masoko na Mawasiliano wa mwezi Juni 2013.<br>- Tathmini ya upatikanaji na usambazaji wa kondomu kwenye maeneo hatarishi katika mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza na Mbeya | |
| Mfumo wa Masoko ya Jumla/kamilifu/jumuishi | - Kuundwa kwa kikundi mahususi cha Mfumo wa Masoko Jumuishi kinacho jumuisha TACAIDS, Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu, Shirika la Umoja wa Mataifa la Kudhibiti UKIMWI, na Mradi Kiongozi Katika Kuimarisha Ushiriki wa Sekta Binafsi katika Afya.<br>- Mikutano ya ushauri ya wadau mbali mbali juu ya masuala ya matumizi ya kondomu kujikinga na maambukizi ya VVU ilifa nyika mwaka 2018<br>- Tafiti mbalimbali zimefanyika ili kuunga mkono Mfumo wa Masoko ya Jumuishi. | - Uunganishwaji finyu wa kanuni za Mfumo wa Masoko Jumuishi kwenye nyaraka za sera za Mkakati wa Taifa wa kondomu.<br>- Upatikanaji na ufikiwaji mdogo wa kondomu katika ngazi yajamii.<br>- Kutokuwepo kwa uhakika wa usafirishaji kwenye sekta ya umma na kumalizika kwa kondomu mara kwa mara kwenye sekta binafsi kumeleta changamoto katika usambazaji<br>- Matumizi finyu ya tafiti kwenye kuratibu kondomu zenye punguzo na za msaada<br>- Kukosekana kwa uratibu katika usambazaji wa kondomu wenye kujenga hali ya uhitajika/katika shughuli za Majadiliano ya mabadiliko ya tabia katika jamii<br>- Muonekano mbaya wa kondomu zilizo kwenye sekta ya umma zinazosaambazwa |

| Kipengele | Mafanikio | Changamoto |
|---|---|---|
| | | nje ya vituo vya afya.<br>- Kukosekana kwa elimu juu ya Mfumo wa Masoko Jumuishi kwa baadhi ya watumishi wa serikali. |
| Usambazaji lengwa | - Uwepo na usambazaji wa waraka na mwongozo wa Taifa wa ugawaji wa kondomu wa mwaka 2029<br>- Usambazaji wa kondomu nje ya vituo vya afya, kupitia utoaji wa huduma mkoba, waelimishaji rika na asasi za kiraia.<br>- Kutumia wasambazaji wa huduma ya uzazi wa mpango katika jamii.<br>- Sekta za masoko jumuishi yanayolenga maeneo hatarishi kama vile baa, hotelini, sokoni, madereva wanaosafiri masafa marefu, n.k. | - Kuwepo kwa uratibu hafifu kati ya sekta za umma, masoko ya kijamii pamoja na sekta ya biashara.<br>- Kushuka kwa kiwango cha asilimia ya watumiaji wa kondomu za sekta ya umma.<br>- Kukosekana kwa mashine za kuhifadhi na kutolea kondomu kwenye maeneo hatarishi na yenye mrundikano wa watu.<br>- Mtazamo hasi na kasumba juu ya matumizi ya kondomu. |
| Mawasiliano ya mabadiliko ya tabia katika jamii. | - Asasi za masoko ya kijamii zinazohamasisha matumizi thabiti ya kondomu.<br>- Uhamasishaji wa matumizi ya kondomu za sekta binafsi kupitia wasambazaji wa kijamii.<br>- Warsha zinazohusu VVU, UKIMWI, na magonjwa ya ngono zikijumuisha elimu juu ya matumizi sahihi na | - Kukosekana kwa rasilimali fedha na watu za kutosha kwa ajili ya programu za kondomu, hususan katika kuchochea mahitaji ya kondomu.<br>- Kukosekana kwa mkakati wa Taifa wa uhamasishaji wa uhitaji/matumizi ya kondomu<br>- Shughuli chache zinahusu uhamasihaji wa matumizi ya kondomu katika jamii |

| Kipengele | Mafanikio | Changamoto |
| --- | --- | --- |
| | endelevu ya kondomu.<br>- Elimu ya Uzazi wa Mpango, ikiwemo elimu juu ya matumizi ya kondomu. | - Upatikanaji hafifu wa nyenzo za kutumia katika uhamasishaji wa matumizi ya kondomu katika ngazi ya jamii.<br>- Bado kuna vikwazo juu ya matumizi ya kondomu katika baadhi ya jamii.<br>- Uaminifu baina ya wapenzi hupunguza kiwango cha matumizi ya kondomu. |

Usalama katika usambazaji wa bidhaa

| Kipengele | Mafanikio | Changamoto |
| --- | --- | --- |
| Mpango wa makisio ya usambazaji | - Makisio ya njia za uzazi wa mpango yalifanywa na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kupitia kitengo cha Huduma ya Afya ya Uzazi na Mtoto.<br>- Mpango wa makisio ya usambazaji unafanyika kupitia Mfumo Jumuishi wa taarifa unaoruhusu vituo vya kutolea huduma za afya kuagiza kwa pamoja dawa, kemikali zinazotumika maabara, na bidhaa mahususi zilizo kwenye programu ikiwemo na kondomu kutegemea mahitaji na bajeti katika vituo husika. | - Kukosekana kwa taarifa za kutosha kwa ajili ya makisio ya Kitaifa.<br>- Utunzaji dhaifu hafifu wa kumbukumbu katika vituo vya kutolea huduma za afya<br>- Kutokuwa na ujuzi wa kutosha kufanya makisio katika vituo vya kutolea huduma ya afya.<br>- Kukosekana kwa ushirikish waji na ujumuishwaji wa kutosha wa sekta ya kondomu za ya bei punguzo na sekta ya biashara katika makisio ya kitaifa. |

| Kipengele | Mafanikio | Changamoto |
|---|---|---|
| Manunuzi | - Bohari Kuu ya Dawa ina uwezo wa kufanya manunuzi ya kimataifa ya kondomu kupitia minada ya wazi yenye ushindani | - Mfumo dhaifu wa ufuatiliaji<br>- Ushirikishwaji hafifu wa wadau kutoka sekta ya soko jamii na na sekta ya biashara katika manunuzi ya kondomu. |
| Udhibiti Ubora | - Uwepo wa hadidu rejea katika mfumo wa udhibiti ubora kwa mamlaka husika.<br>- Uwepo wa utaratibu wa kufanya upimaji wa kondomu baada ya kuwa uzalishwaji ambapo maabara hupima fungasho za kondomu 4-5 kwa siku.<br>Uwepo wa maabara 6 za viwango vya juu vya ubora wa ISO 9001 zilizothibitishwa ikiwemo za kupima ubora wa kondomu.<br>- Uwepo wa kifaa kinachoongeza uwezo wa upimaji kwenye mfumo.<br>- Uwepo wa chapa/aina mbalimbali za kondomu za kiume, na aina/chapa moja ya kondomu ya kike zilizosajiliwa nchini<br>- Kondomu zimesajiliwa kama kifaa tiba daraja "C"<br>- Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba hutoa kibali ndani ya saa 48 ambacho | - Mamlaka husika hutumia muda mrefu kutoa mrejesho wa matokeo baada ya upimaji wa shehena za kondomu. |

| Kipengele | Mafanikio | Changamoto |
|---|---|---|
| | hudumu kwa miezi sita. Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba hufanya utafiti wa masoko ya kondomu baada ya upimaji kujiridhisha na ubora | |
| Mnyororo wa usambazaji katika sekta ya umma | - Bohari Kuu ya Dawa ina uwezo wa kuhifadhi kondomu kwenye gala la taifa na za Kanda.<br>- Uwepo wa Mfumo wa Usimamizi wa Taarifa umesaidia kuboresha mfumo wa uagizaji.<br>- Usambazaji jumuishi wa kondomu kwenye vituo vya afya na zaidi ya hapo.<br>- Kuingizwa kwa kondomu kwenye orodha ya vifaa tiba muhimu.<br>- Ujumuishwaji wa kondomu kwenye miongozo yote ya afua za VVU na UKIMWI. | - Kondomu kama kifaa tiba inasababisha ucheleweshaji wa usambazwaji na upatikanaji nje ya vituo vya kutolea huduma ya afya (kwenye jamii).<br>- Kumeripotiwa uhaba wa kondomu wa mara kwa mara katika vituo vya afya<br>- Vituo vya kutolea huduma ya afya havina utaratibu/mfumo wa kusambaza kondomu nje ya eneo la kazi.<br>- Kutokuwepo utaratibu wa usambazaji wa kondomu kwenye idara na sekta nyingine zza umma ngazi ya taifa, mkoa na wilaya. |

**2.8.3** Kazi saidizi za kuratibu programu za kondomu

| Kipengele | Mafanikio | Changamoto |
|---|---|---|
| Uimarishaji wa uwezo na taasisi | - Uimarishaji wa uwezo wa sekta binafsi na sekta ya soko jamii. | - Uwezo finyu wa taasisi kwenye kuratibu programu za kondomu zinahusu mafunzo kwa wakufunzi.<br>- idara, Mawakala, taasisi za serikali na wadau mbalimbali.<br>- Usambazaji hafifu wa taarifa miongoni mwa Asasi za Kiraia. |

| Kipengele | Mafanikio | Changamoto |
|---|---|---|
| Ufuatiliaji na tathmini | - Kondomu hufuatiliwa kupitia ripoti za Utafiti wa Viashiria vya VVU na UKIMWI na Malaria/ Utafiti wa viashiria vya Afya na Makazi (nyaraka ya Uzazi wa Mpango, Uzuiaji wa maambukizo wa VVU Kutoka kwa Mama kwenda kwa Mtoto, Tiba, pamoja na Unasihi na Upimaji wa Hiari pamoaja na ripoti ya Mfuko wa Ufuatiliaji wa Mafanikio ya Mapambano dhidi ya UKIMWI<br>- Kuimarisha mfumo wa ripoti kama iliyobainishwa kwenye miongozo ya usambazaji wa kondomu. | - Kuna mfumo duni wa ufuatiliaji na tathmini ya programu za kondomu kutokana na kukosekana kwa ushiriki wa rasilimali watu pamojan na kukosekana kwa upatikanaji wa uchambuzi na uhifadhi wa takwimu wa pamoja<br>- Kukosekana kwa muunganiko ndani ya Mfumo wa Usimamizi wa Taarifa zinazohusu matumizi ya kondomu katika sekta ya masoko na makampuni ya kijamii, na sekta ya biashara. |
| Uhifadhi wa programu, michakato, maendeleo na matokeo. | - Uhifadhi unaoendelea kufanywa na asasi mbalimbali. | - Kukosekana kwa mbinu rasmi za na za pamoja za uhifadhi katika kusambaza taarifa zinazohuu uboreshaji wa programu. |

## SEHEMU YA 3: LENGO, DHUMUNI, MATOKEO NA MIONGOZO ELEKEZI

### 3.1 Lengo

Lengo la Mkakati wa Taifa wa Kondomu ni kubainisha vipaumbele vya kimkakati vinavyohitajika katika kupunguza maambukizi ya VVU, maambukizi kupitia ngono, pamoja na mimba zisizotarajiwa nchini Tanzania.

### 3.2 Dhumuni

Dhumuni la Mkakati wa Taifa wa Kondomu kama lilivyobainishwa katika Mkakati wa nne wa Taifa wa Kudhibiti VVU na UKIMWI, na Mpango wa Taifa wa Utekelezaji wa Uzazi wa Mpango Uliohuishwa ni kuhakikisha kunakuwa na matumizi sahihi na endelevu ya kondomu kama kinga dhidi ya VVU na maambukizo kupitia ngono, pamoja na mimba zisizotarajiwa nchini Tanzania,


i. **MATUMIZI**: Kiwango cha asilimia ya matumizi ya kondomu kimeripotiwa kuongezeka miongoni mwa wanaume na wanawake.
ii. **UENDELEVU**: Kuongezeka kwa kiwango cha ubora na kiasi kwenye soko la kondomu
iii. **USAWA**: Kuhakikisha upatikanaji na wenye gharama nafuu wa kondomu.

### 3.3. Matokeo ya kimakakati

Matokeo ya kimkakati yanayowiana na maeneo muhimu ya vipaumbele ni:

- Uboreshaji wa uongozaji na uratibu wa kondomu
- Uongezekaji wa Usambazaji na Uhakika wa bidhaa
- Uboreshaji wa uhitaji, ufikiaji na utumiaji
- Uratibu wa program wezeshi

**Jedwali la 4: Mfumo wa jumuishi wa kuratibu programu za kondomu**




### 3.4 Kanuni elekezi

Kanuni elekezi za Mkakati wa Taifa wa kondomu ni:

i. **Udhibiti thabiti wa VVU na UKIMWI**: Shughuli zitakazofanyika zitajikita kwenye utafiti pamoja na masuala yanayohamasisha matumizi sahihi ya kondomu

ii. **Upatikanaji wa kondomu kama haki ya binadamu:** Ni lazima kondomu zipatikane kwa urahisi kwa wote bila kujali kabila, jinsi, ulemavu, mitazamo ya kisiasa, hali ya kiuchumi, hali ya kijamii, au makazi. Ni lazima programu zinazohusu kondomu zilinde na kuheshimu haki za wateja na familia zao, pamoja na watoa huduma.

iii. **Usambazaji lengwa (ukijumuisha makundi maalumu na yaliyo katika mazingira hatarishi)**: Ni lazima msisitizo ulenge katika kuwezesha upatikanaji rahisi wa kondomu pamoja na kuondoa vikwazo vinginevyo vinavyokwamisha upatikana kwa ajili ya makundi mbalimbali yaliyo katika hatari zaidi au mazingira hatarishi wakiwemo wanaofanya biashara ya ngono, wanaume wanaofanya ngono na wanaume wenzao, watu wanaojidunga madawa ya kulevya, wanaotumia dawa za kulevya, LDTD, wafanyakazi wa migodini, wavuvi, na wafungwa magerezani, n.k

iv. **Mwitikio wa kijinsia**: Programu za kondomu zinapaswa kuingiza masuala ya uinsia katika mipango na utekelezaji. Msisitizo unapaswa kuwa kwenye kuwasaidia wanawake kushiriki ipasavyo kwenye kutoa maamuzi juu ya matumizi ya kondomu.

v. **Upatikanaji na uwezo wa kumudu gharama za kondomu**: Mkakati utalenga kuboresha suala la zima la upatikanaji wa kondomu, ukizingatia uwezo wa watumiaji kumudu gharama.

vi. **Mfumo jumuishi na uratibu:** Mkakati huu unahimiza, mifumo iliyopo katika ngazi ya kijiji, vituo na asasi zinazofanya kazi ya uratibu zitashughulikia masuala mahususi ikiwemo kondomu katika jamii.

vii. **Ushirikishwaji kisekta**: Mkakati unajumuisha wadau mbalimbali kutoka serikalini, Asasi za Kiraia, wabia wanaotekeleza, pamoja na sekta za biashara katika mipango na utekelezaji wake.

viii. **Mfumo wa Masoko Jumuishi**: Lengo kuu kwenye masoko jumuishi ni kuleta ufanisi wa shughuli ikiwa ni pamoja na kuboresha masoko endelevu. Shughuli za manunuzi na usambazaji wa kondomu za punguzo na za bure zinapaswa kuwianishwa na makadirio halisi ya uhitaji, pamoja na kuungwa mkono na uwekezaji katika majadiliano ya mabadiliko ya tabia katika jamii na uhamasishaji wa kondomu.

**Kanuni za Mfumo wa Masoko ya Jumuishi**: Mkakati unatekeleza kanuni za Mfumo wa Masoko Jumuishi zenye lengo la kuwashirikisha wadau wanaoratibu programu za kondomu, wakati huohuo unajikita kwenye maeneo yafuatayo:

- **Faida linganifu:** Wadau/wahusika wanapaswa kufanya kazi pamoja kama timu ili kuhakikisha kwamba, wanatoa huduma kwa wateja wote, na wanakidhi malengo ya afya kwa umma.
- **Chaguo la mteja**: Mfumo wa Masoko Jumushi inatambua kwamba wateja wanaweza kuchagua wasambazaji wanaokidhi mahitaji yao kwa kiwango cha juu kama vile; ladha, aina ya bidhaa, na uwezo wa kumudu gharama za manunuzi.
- **Uhuru wa wasambazaji**: Ingawa serikali inaratibu na kusimamia Mkakati wa Masoko ya Jumuishi, wadau mbalimbali katika masoko wanao uhuru wa kutekeleza au kutokutekeleza mkakati huu.
- **Thamani ya Pesa**: Mfumo wa Masoko Jumushi unaweza kuwekeza fedha kutoka kwa wadhamini katika namna inayounga mkono masoko endelevu, na kuziwezesha sekta za biashara kufikia lengo la kuongeza gawio la uhitaji wa kondomu

## SEHEMU YA 4: MIKAKATI YA UTEKELEZAJI

Maeneo muhimu ya vipaumbele yaliyobainishwa ndiyo matokeo ya Mkakati wa Taifa wa Kondomu. Kipengele hiki kinaelezea kwa kina vipaumbele vya kimkakati vilivyo pendekezwa katika kushughulikia changamoto zilizobainishwa wakati wa uchambuzi.

### 4.1 Uboreshaji wa Uongozi na Uratibu.

#### 4.1.1 Uratibu wa Wadau

Uratibu wa programu za kondomu utakuwa chini ya Kamati shirikishi ya Kitaalamu ya kudhibiti VVU na UKIMWI. Kamati shirikishi ya kondomu itasimamiwa kwa pamoja na TACAIDS na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, chini ya Mpango wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI. Mmoja kati ya Wadau ambaye ni mjumbe ndani ya Kamati shirikishi ya Kitaalam atakuwa katibu wa Kamati. Wizara, Idara Zinazojitegemea na Wakala za Serikali na Wabia wa Maendeleo, pamoja na Wabia Watekelezaji wengine watakuwa wajumbe wa Kamati shirikishi ya kondomu. Hata hivyo, ili kujenga ushirikiano na uratibu imara, mwenyekiti wa kamati shirikishi ya kondomu atakuwa mjumbe wa kamati ya Usalama wa bidhaa za Afya ya Uzazi. Kamati shirikishi ya kondomu itahakikisha kunakuwa na uratibu wa kina katika programu za kondomu kwa kushirikiana na wadau, vilevile itaweka ajenda za programu za kondomu na kuwa washauri kwenye masuala ya sera.

Lengo mahususi la kamati shirikishi ya kondomu itakuwa kutengeneza muungano kati ya Kinga dhidi ya VVU, magonjwa mengine maambukizi mengine ya magonjwa ya Ngono na njia za uzazi wa mpango. Pia, kuhakikisha kwamba, wale wabia wanaotekeleza Mkakati wa Kondomu wanaratibiwa kimkakati. Ili kuhakikisha kunakuwa na Kinga madhubuti, utoaji na usambazaji wa kondomu itakuwa ni jukumu la Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kupitia Huduma ya Afya ya Uzazi na Mtoto na Mpango wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI. Taasisi hizi za Serikali, TACAIDS, Mpango wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI, Huduma ya Afya ya Uzazi na Mtoto, (Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto) Wabia wa Maendeleo na Wabia Watekelezaji watashirikiana kutoa msaada kwenye mikutano ya robo mwaka ya kamati shirikishi ya kondomu, pamoja na uendeshaji wa mpango kazi.

**Vipaumbele vya kimkakati:**

1. Kuimarisha kamati shirikishi ya Taifa ya kondomu ikiwa ni pamoja na kubainisha kwa ufasaha hadidu za rejea, kukuza uanachama, mpango kazi wa mwaka wa kamati, mapato na matumizi.

2. Kuhakikisha kuwa mahitaji ya kondomu kuanzia upokeaji, usambazaji, pamoja na utoaji wa taarifa zinakuwa moja kati ya ajenda za kudumu za Kamati kuanzia ngazi ya Taifa, Mkoa Halmashauri, Kata na Mtaa/kijiji kupitia mfumo wa uratibu uliopo.
3. Kujenga muungano pamoja na mahusiano mazuri ya kazi kati ya sekta za afya na sekta zingine zote katika ngazi zote, ikiwa ni pamoja na kuwianisha na kuratibu wabia ili kurahisisha utekelezaji wa mkakati wa kondomu.
4. Kuchukua na kutekeleza kanuni za Mfumo wa Masoko Jumuishi za programu za kondomu nchini.
5. Kutumia mikutano ya kidini na majukwaa ya viongozi wa kisiasa katika kushughulikia vipaumbele vya kimakakati vilivyounganishwa kwenye mkakati wa Taifa wa kondomu.

#### 4.1.2 Uraghibishaji wa Rasilimali

Uhamasishaji wa mabadiliko ya sera na udhibiti katika kuimarisha mazingira wezeshi ya programu za kondomu utakuwa ndiyo msingi bora na thabiti katika Nyanja za kisiasa na kijamii katika matumizi ya kondomu. Aidha, matumizi sahihi na endelevu ya kondomu miongoni mwa wanaume na wanawake inategemea na uhakika wa kukubalika, upatikanaji na gharama nafuu za kondomu na vilainishi vya kondomu.

Kwa uhakika wa upatikanaji wa kondomu, serikali na wadau wanatakiwa kuwa na mpango na bajeti ya kondomu za ruzuku na za biashara kwenye sekta zote za umma na binafsi nchini. Hii inaweza kutokana na bajeti ya afya, Mfuko wa msaada wa VVU na UKIMWI, au vyanzo vingine. Serikali inatambua mchango wa wadau watekelezaji na itaendelea kushirikiana nao ili kuhakikisha kuwa kondomu zenye punguzo zinapatikana. Hata hivyo, ni muhumu sana kuwa na mpango wa uendeshaji wa mkakati wa kondomu ili utumike kama chombo katika ukusanyaji wa rasilimali.

**Vipaumbele vya kimakakati:**

1. Kuanzisha uchambuzi wa sera na udhibiti, pamoja na mijadala inayohusu programu za kondomu.
2. Kutambua na kuimarisha wahamasishaji walio katika maeneo ya kisiasa, kidini na kijamii.
3. Kujenga umoja na ubia na asasi za kiraia na kijamii, sekta binafsi na zisizo rasmi pamoja na nyanja zingine za kijamii.
4. Kuhakikisha kuwa kunakuwa na fedha pamoja na rasilimali za kutosha katika usambazaji na utekelezaji wa mkakati wa kondomu, na kwa ajili ya manunuzi ya kondomu za ruzuku na biashara.

## 4.2 Uboreshaji wa usambazaji na uhakika wa bidhaa

### 4.2.1 Mpango wa makisio ya usambazaji wa kondomu.

Katikia kipindi cha nyuma mpango wa makisio ya usambazaji ulitegemea sana takwimu za kihistoria kutoka sekta ya afya tu. Ni muhimu sasa kuzingatia sekta zote ikiwa ni pamoja na masoko ya kijamii, makampuni ya kijamii, sekta ya biashara kwa ajili ya mahitaji ya kondomu kwa wote. Waingizaji wote wa kondomu ikiwa ni pamoja na masoko ya kijamii, makampuni ya kijamii na sekta za biashara wanapaswa kushiriki katika makadirio ya upigaji wa mahesabu ya idadi ya kondomu. Kunapaswa kuwa na Upigaji wa mahesabu ya kondomu ya mara kwa mara ili kushughulikia mahitaji ya kudhibiti wa VVU na UKIMWI pamoja na kuzuia mimba zisizotarajiwa nchini.

Makisio yanapaswa kufikia mpango wa miaka mitatu wa usambazaji unaoshughulikiwa na masoko ya sekta ya umma, masoko na makampuni ya kijamii, pamoja na sekta za biashara. Mpango wa usambazaji utakuwa ndiyo msingi wa ukusanyaji wa rasilimali ili kuhakikisha kuwa makadirio ya uhitaji ndiyo yatakayotumika kuagiza kondomu kutoka kwenye gala za mkoa.

**Vipaumbele vya kimkakati:**

1. Kuhakikisha kuwa kunakuwa na uboreshaji wa makisio, idadi, na mpango wa usambazaji wa kondomu utakaozingatia sekta zote zikiwemo masoko ya kijamii, makampuni ya kijamii na sekta za biashara.
2. Kufanya utambuzi wa mahitaji ya usambazaji wa kondomu kupitia makisio halisi ya mahitaji.
3. Kuingiza Mfumo ya Masoko ya Jumla katika ngazi mbalimbali za Serikali ili kufanikisha uelekezwaji wa idadi wa kiwango cha juu wa kondomu, pamoja na ugawaji wa kondomu za bure, ugawaji fasaha wa kondomu zenye punguzo, pamoja na ukuzaji wa bei imara ya chapa/aina za kondomu.
4. Kuhakikisha kuwa utunzaji wa kumbukumbu za kondomu na utoaji wa taarifa vinafanywa katika ngazi zote ikiwemo sekta ya masoko ya kijamii na sekta ya biashara.

5. Kuhakikisha kuwa watoa huduma za afya na rasilimali watu kutoka sekta na asasi zingine wanapewa stadi/ujuzi juu ya kutambua mahitaji ya kondomu.

### 4.2.2 Mfumo wa Usimamizi wa Taarifa

Vyanzo vikuu vinavyotakiwa kwa ajili ya mfumo fasaha/fanisi wa usambazaji wa kondomu ni pamoja na suala la kumbukumbu za miamala na utunzaji wa bidhaa. Ni muhimu kwa sekta zote za umma kuhakikisha kwamba vituo vyote vya afya vinahifadhi kadi ya bidhaa ya kondomu pamoja na masuala ya takwimu, ikiwa ni pamoja na masuala ya kumbukumbu zilizo nje ya vituo vya afya. Ni lazima kuwe na mbinu ya upataji wa taarifa za kondomu katika ngazi ya taifa kwa madhumuni ya makadirio na mipangilio. Kunatakiwa kuwe na uwezo wa kufungua, kuwa nayo na kutumia kadi ya bidhaa ya kondomu katika vituo vya afya. Ripoti za mara kwa mara za kitaifa juu ya kondomu zilizopo na zilizopita muda wa matumizi.

**Vipaumbele vya kimkakati:**

1. Kuimarisha na kukuza Mfumo wa Jumuishi wa Taarifa ili kuweza kukusanya takwimu za kutosha na bora kwa ajili ya makisio ya kondomu.
2. Kukuza Mfumo wa Kielektroni wa Usimamaizi wa Taarifa ili kuwezesha upatikanaji fasaha wa takwimu za kondomu.
3. Kuimarisha usimamizi wa mfumo wa usambazaji wa kondomu katika ngazi zote ili kuhakikisha upatikanaji na unafuu wa bei ya kondom kwa watu wanaohitaji.
4. Utekelezwaji wa mfumo wa manunuzi wa kondom

### 4.2.3 Kuongeza usambazaji wa kondomu kupitia mitandao ya sekta binafsi, masoko ya kijamii, na sekta za biashara

Uchukuaji wa kondomu unategemea sana upatikanaji wa kondomu katika sehemu husika kwa ajili ya makundi lengwa. Ili kuhakikisha kuwa uhitaji wa kondomu ni wa kuridhisha, ni lazima kupanua wigo wa usambazaji wenye ufanisi wa hali ya juu kwenye vituo vilivyo nje ya sekta ya afya ya umma katika jamii, kwenye maduka ya rejareja na kwenye sekta ya biashara kama vile baa na hoteli. Serikali ya Tanzania itashirikiana na wadau wote wa masoko ili kupanua kimkakati vituo na aina ya usambazaji wa kondomu. Ili kuhakikisha kuwa inakuwa na utekelezaji wa uhakika, Serikali kupitia Mkakati wa Kondomu uliotayarishwa utayagawanya masoko na kuchukua Mfumo wa Masoko Jumuishi ili kuruhusu wadau kuwa katika nafasi nzuri ya kuhudumia kundi lengwa ili kuinua huduma zake.

Vilevile itahakikisha uwepo wa sehemu za kutosha za kuhifadhia kondomu kwa ajili ya sekta ya afya katika ngazi ya Taifa, ghala za mkoa. Asasi za masoko ya kijamii, na sekta za biashara zinakuwa na mfumo madhubuti wa uhifadhi na usambazaji. Uwepo wa miongozo ya Taifa ya usambazaji wa kondomu inayoelekeza namna ambavyo kondomu zitasambazwa kwenye vituo vya afya na katika maeneo mengine zikiwemo sekta zote. Usambazaji wa

kondomu katika sekta ya umma kupitia vituo vya sekta ya jamii na binafsi kunaleta hatari ya upunguaji wa mauzo ya kondomu katika masoko ya kijamii, makampuni ya kijamii pamoja na sekta ya biashara, kwa sababu hiyo, ni muhimu ifuatiliwe kwa makini na iungwe mkono kwa miongozo mahususi inayobainisha jukumu la kila mhusika.

**Vipaumbele vya kimkakati:**

1. Kuhakikisha kuwa, mbinu za usambazaji wa kondomu, uagizaji, ufikishaji, uhifadhi pamoja na taarifa zinazohusu matumizi ya kondomu zinaunganishwa na miongozo ya Taifa ya usambazaji wa kondomu.
2. Kuunganisha uwekezaji wa mawasiliano ya mabadiliko ya tabia katika jamii na uhamasishaji wa matumizi ya kondomu kwenye malengo ya afya ya umma.
3. Kuhakikisha kuna upatikanaji wa kondomu kwenye vituo vyote na mifumo yote ya usambazaji.
4. Kuhakikisha kunakuwa na uboreshaji wa upatikanaji na mahusiano kati ya sekta binafsi, masoko ya kijamii, makampuni ya kijamii na sekta za biashara za kondomu, kwa kutumia mitandao mikubwa ya sekta binafsi.
5. Kutumia kanuni za Mfumo wa Masoko Jumuishi wakati wa kugawa na kusambaza kondomu kwa wahusika/wadau wote wa usambazaji wa kondomu.

### 4.3 Uhitaji, Upataji na Utumiaji

#### 4.3.1 Usambazaji wa Kondomu kwa walengwa

Ili kuongeza kiwango cha matumizi ya kondomu ni muhimu kubainisha makundi lengwa, na kuzipambanua sifa zao mahususi kwa kutumia mbinu madhubuti kwa kulenga makundi maalumu kutaongeza hamasa na ufanisi wa Afua. Hii ni kwa sababu, kuzielekeza afua kwa makundi lengwa, ambapo ushamiri wa kiwango cha matumizi ya kondomu kutaleta faida katika kudhibiti na kukinga VVU na UKIMWI, kutatokomeza maambukizi ya VVU kwa kiwango kikubwa, pamoja na kukinga mimba zisizotarajiwa. Pamoja na hayo, Kwa kulenga makundi maalumu kutaruhusu watekelezaji kutayarisha afua kwa kutumia njia na nyenzo sahihi kwa kila kundi, hivyo kuongeza ufanisi wa afua.

Kwa ujumla, msisitizo wa mfumo wa masoko ya jumla ya kondomu utakuwa kwa wanaume na wanawake wote wenye uwezo wa kushiriki ngono. Hata hivyo, wafuatao wamebainiwa kuwa makundi lengwa, ikiwa ni pamoja na makundi yaliyo katika hatari kubwa ya kusambaza au kupata VVU kama yalivyobainishwa kwenye ripoti ya uchunguzi wa haraka wa programu za kina za kondomu:

- Watu wazima na vijana wanaoshiriki ngono ya wapenzi wengi;

- Wanaume na wanawake wanaofanya biashara ya ngono na wateja wao;
- Watu wazima wanaofanyakazi mbali na familia zao kama vile wafanyakazi wanaosafiri na wale wa kuhamahama, vibarua, wachimbaji wa madini, wafungwa magerezani, madereva wanaosafiri masafa marefu, jamii za wavuvi, n.k;
- Watu wazima na watoto wanaopata huduma za uzazi wa mpango pamoja na huduma za kujifungua;
- Wakimbizi wa ndani na nje ya nchi;
- Watu wanaojidunga dawa za kulevya, wanaume wanaofanya ngono na wanaume wenzao, na wafanya biashara ya ngono;
- Wasichana balehe na wanawake vijana.

Ili kukidhi mahitaji ya makundi yote, kuna umuhimu wa kutumia mikakati ya masoko ya jumla, ikiwa ni pamoja na mgawanyiko mahususi ili kuongeza kiwago cha matumizi ya kondomu.

**Vipaumbele vya kimkakati:**

1. Kuhakikisha ugawaji wa miongozo inayohusu usambazaji wa kondomu kwa wadau wote.
2. Kusimamia tafiti za soko la kondomu ili kuelewa mahitaji na machaguo/mapendeleo ya kondomu miongoni mwa makundi lengwa yaliyo katika jamii, yakiwemo makundi yaliyo katika hatari zaidi. Mfano: wasichana balehe na wanawake vijana, kundi la vijana, wanawake wanaofanya biashara ya ngono, wanaume wanaoshiriki ngono na wanaume wenzao, wanawake na wanaume, watu wanaojidunga dawa za kulevya, watu wanaotumia dawa za kulevya, wachimbaji wa madini, pamoja na taasisi za elimu ya juu.
3. Kuhakikisha kunakuwa na ongezeko la kiwango cha ujuzi/uelewa juu ya kinga dhidi ya VVU kwa makundi lengwa mbalimbali yaliyo katika jamii ili kupunguza imani na fikra potofu zinazohusiana na matumizi ya kondomu.
4. Kuongeza kiwango cha usambazaji wa kondomu katika ngazi zote.
5. Kushirikisha Asasi za Kiraia, mabaraza ya wazee, makundi ya WAVIU na wasio WAVIU yenye umri na jinsia zote, kama vile Vijana, pamoja na Wanaume na Wanawake Watu wazima, ili kutengeneza hali ya uhitaji wa matumizi ya kondomu.
6. Kuhakikisha upatikanaji wa mashine ya kuweka na kutolea kondomu katika vituo mbalimbali.

### 4.3.2 Mfumo wa Masoko ya Jumuishi katika kuongeza kiwango cha upataji wa kondomu

Mipango ya programu za kondomu zitatumia mfumo wa masoko ya jumla, ambapo kondomu zitapatikana kupitia mifumo/njia za sekta za umma, binafsi na za kibiashara. Watu hubadili aina ya kondomu kutegemea na hali/mazingira, kondomu katika sekta za umma zinapaswa kuwalenga wanaume na wanawake walio katika hali ya chini ya kijamii na kiuchumi. Watu ambao hawawezi kumudu gharama za kondomu, wanaoishi katika maeneo ambayo yana ugumu wa kununua au kupata kondomu aina ya Salama zenye punguzo wanahitajika kupewa kondomu za sekta ya umma ambazo zinatolewa bila malipo. Walengwa wa pili wa kondomu hizi ni pamoja na wanawake wanaofanya biashara ya ngono, wanaume wanaoshiriki ngono na wanaume wenzao, vijana balehe, vijana na makundi mengine maalumu na yaliyo katika mazingira hatarishi katika nyanja ya elimu na programu za nje bila kujali hali ya kijamii au ya kiuchumi.

Usambazaji wa kondomu katika sekta ya umma utaimarishwa na sekta ya masoko ya kijamii, makampuni ya kijamii, na sekta za biashara kwa kuziba mapengo ambayo hayawezi kuzibwa na sekta ya umma kutokana na uwezo au rasilimali. Kwa gharama ya sekta za biashara ya kondomu, sekta ya masoko ya kijamii na makampuni ya kijamii ya kondomu zitaziba pengo ambalo sekta za biashara hazitaliziba kwa sababu hazifaidiki sana katika kuifanya kama biashara. Pia, sekta ya masoko ya kijamii ya kondomu italenga wale wanaoweza kulipa gharama ya kawaida na wale wasiojiweza, pamoja na makundi yaliyo katika hatari kubwa na yale yaliyo katika mazingira hatarishi. Mikakati mahususi ya masoko kulenga makundi haya itaboreshwa kila baada ya miaka miwili kwa kila toleo/aina ya kondomu, vilevile itagawiwa miongoni mwa wadau kulingana na mikakati ya uhitaji na usambazaji wa kondomu itakayotumika.

### 4.3.3 Utekelezaji wa Mfumo wa Masoko Jumuishi: Majukumu na Wajibu katika ngazi mbalimbali

| Ngazi | Majukumu na Wajibu |
|---|---|
| Ngazi ya Taifa<br>• TACAIDS,<br>• Mpango wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI,<br>• Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za | • Kutengeneza sera na miongozo inayojumuisha takwimu na matokeo ya tafiti, sambamba na kutumia kwa ufasaha rasilimali za umma.<br>• Kuunganisha kanuni za mifumo ya masoko ya jumla kwenye programu za kondomu kupitia Kamati shirikisha za kondomu, kikundi kazi cha kitaalamu cha usalama wa bidhaa, pamoja na kikundi kikuu cha sekta binafsi ya |

| Ngazi | Majukumu na Wajibu |
|---|---|
| Mikoa na Serikali za Mitaa | Uzazi wa Mpango.<br>• Kushirikiana na sekta binafsi, ikiwa ni pamoja na asasi za masoko ya kijamii, makampuni ya kijamii na asasi za kijamii ili kukuza sera ya kondomu.<br>• Kufanya kazi na Wabia wa Maendeleo ili kuhakikisha kwamba ununuzi na mpango wa kujenga hali ya uhitaji wa kondomu/ programu za maasiliano ya mabadiliko ya tabia katika jamii unadhaminiwa vya kutosha.<br>• Kuratibu na kusimamia usimamizi na uongozaji wa maendeleo katika ngazi ya mkoa. |
| Ngazi ya Wilaya<br>• Mratibu wa Kudhibiti UKIMWI wa Wilaya<br>• Mratibu wa Afya ya Uzazi na Mtoto wa Wilaya<br>• Mratibu wa VVU NA UKIMWI wa Halimashauri | • Ainisha mahitaji ya kondomu pale inapohitaji kwa kutumia vyanzo vyote vya taarifa vilivyopo.<br>• Fuatilia na toa taarifa juu ya matumizi ya kondomu zilizogharamiwa na Serikali ikijumuisha usambazaji wa kondomu nje ya vituo vya afya.<br>• Kuratibu usambazaji wa kondomu kwa kuzingatia hali ya kuhitaji wa kondomu.<br>• Kushirikiana na wasambazaji wa kijiji wa sekta za biashara na asasi za masoko ya biashara ili kuelewa vyema shughuli zao, mikakati ya usambazaji na kiwango chao cha mauzo. |
| Ngazi ya kituo cha afya<br>• Msimamizi wa Kituo<br>• Mfamasia<br>• Msimamizi wa afya ya uzazi na mtoto<br>• Msimamizi wa kituo cha Unasihi na Upimaji<br>• Msimamizi wa bohari | • Kuhakikisha kwamba kondomu zilizotolewa kwa msaada zinatumika kule zinapohitajika kutumika.<br>• Kuratibu usambazaji wa kondomu kwa kutengeneza hali ya mahitaji ya kondomu kwa lengo la kuleta mabadiliko ya tabia kwenye jamii.<br>• Fuatilia na toa taarifa juu ya matumizi ya kondomu katika vituo na nje ya vituo vya afya. |

| Ngazi | Majukumu na Wajibu |
|---|---|
| Asasi za Kiraia<br>• Waratibu<br>• Mawasiliano ya kubadili tabia kaika jamii<br>• Wasimamaizi/Afisa | • Kutumia takwimu zilizopo wakati wa makadirio ya mahitaji ya kondomu.<br>• Kulenga bidhaa zilizotolewa bure/kwa msaada kwa wanaozihitaji zaidi.<br>• Kushirikiana na wasambazaji wa kijiji wa sekta za biashara, asasi za masoko ya biashara ili kuelewa vyema shughuli zao, mikakati ya usambazaji na kiwango chao cha mauzo, pamoja na kukwepa marudio ya kazi.<br>• Kushirikiana na sekta zingine (hasa wasambazaji wa sekta za biashara, asasi za masoko ya kijamii, na makampuni ya kijamii) wakati wa kusambaza idadi kubwa ya kondomu kwa makundi yaliyo vijijini. |

**Vipaumbele vya kimkakati:**

1. Kuwezesha uratibu wa makundi lengwa kwa sekta za masoko ya kijamii, sekta za umma na sekta za biashara za kondomu ili kukuza kiwango cha matumizi ya kondomu.
2. Kutengeneza mazingira wezesha yanayoruhusu watu wenye nguvu za kushiriki ngono bila kujali umri, jinsia makazi, miongoni mwa vitambuzi vingine vya makazi ili kupata kondomu zenye ubora.
3. Kuhakikisha utekelezaji wa kanuni za Mfumo wa Masoko Jumuishi zinazowezesha kila mhusika/mdau kuratibu jitihada wakati wakikidhi malengo mahususi ya afya.
4. Kuanzisha Tatifi endeshaji za Taifa ili kutoa taarifa za masoko kupitia takwimu za umma na tafiti za masoko.

### 4.3.4 Mawasiliano ya Mabadiliko ya Tabia katika Jamii kwa ajili ya matumizi ya kondomu

Mikakati thabiti ya majadiliano ya Mabadiliko ya Tabia katika Jamii itatumika kushughulikia vikwazo vinavyohusiana na matumizi ya kondomu miongoni mwa makundi lengwa. Kampeni zinazohusu mawasiliano ya kukuza uelewa juu ya VVU, Afya ya Jinsia na Uzazi zitalenga hasa makundi lengwa. Kwa kuzingatia kwamba afua za kijamii zinaweza kuwa ni fasaha na tulivu kwa mtu binafsi, vituo vitapaswa kuchaguliwa kiumakini zaidi. Mitandao ya kijamii na mawasiliano ya kidigitali inapaswa kutambuliwa kama njia ya mawasiliano ya

muhimu na inayokua kwa haraka, hasa inapolenga vijana walioko mijini. Wakati viongozi rika na wasambazaji wa kijamii ni njia muhimu sana, ni muhimu wakatumiwa kwa ajili ya makundi yaliyo vijijini, makundi maalumu na makundi ambayo ni magumu kuyafikia au yanakumbana na vikwazo vya kijamii na kiutamaduni juu ya matumizi ya kondomu.
Matumzi ya kondomu yatahamasishwa kwa ujumbe mahususi na uhamasishaji wa kijamii ili kutengeza mazingira wezeshi kwa ajili ya mabadiliko ya tabia.

**Vipaumbele vya kimkakati:**

1. Kuhamasisha utekelezaji fasaha wa utengenezaji wa uhakika wa hali ya uhitaji wa kondomu katika ngazi zote pamoja na makundi lengwa na kuhakikisha kunakuwa na matokeo thabiti.
2. Kuhakikisha kunakuwa na upatikanaji wa tathmini thabiti katika uboreshaji wa mahitaji na matumizi ya kondomu kama kigezo katika vikwazo vya mabadiliko ya Tabia
3. Kuimarisha elimu na taarifa juu ya kondomu kwa vijana, ikiwa ni pamoja na makundi maalumu na yaliyo katika mazingira hatarishi.
4. Kuongeza uhamasishaji wa matumizi sahihi na endelevu ya kondomu katika ngazi zote.
5. Kuamsha ari ya uhamasishaji wa kijamii katika jamii ili kuhakikisha kunakuwa na mazingira stahiki ya kondomu za kike na za kiume.
6. Kuhakikisha kunakuwa na uchambuzi wa mgawanyiko wa kondomu pamoja na watumiaji.
7. Kutuma ujumbe wa kuwawezesha wanawake kuwa na ujuzi/uelewa wa majadiliano juu ya matumizi ya kondomu, mila za kijamii na matumizi sahihi na endelevu ya kondomu
8. Kushughulikia imani na fikra potofu juu ya matumizi ya kondomu.
9. Kutumia teknolojia ya mtandao pamoja na wahamasishaji (kutengeneza Programu za Simu, matangazo ya mtandao na mitandao ya kijamii ili kuongeza kiwango cha upataji na matumizi ya kondomu).
10. Kuhamasisha upataji wa kondomu katika taasisi za elimu ya juu (Vyuo vishiriki/ Vyuo Vikuu, n.k)
11. Kushirikisha sekta binafsi, masoko ya kijamii, makampuni ya kijamii na sekta za biashara za kondomu.

### 4.4 Majukumu ya mipango ya programu na Msaada

#### 4.4.1 Tafiti, Ufuatiliaji na Tathmini

Mkazo unapaswa kuelekezwa kwenye utekelezaji wa tafiti za kijamii, tabia na uendeshaji ili kutoa matokeo yanayoweza kutoa taarifa na muongozo katika maendeleo na utelekelezaji wa programu. Ajenda ya Utafiti wa Taifa wa VVU na UKIMWI Tanzania (2013-2015)[28], ulibainisha mahitaji machache ya utafiti wa programu za kondomu. Tafiti za uboreshaji wa programu za kondomu zinapaswa kupewa kipaumbele na kuratibiwa ipasavyo. Mkakati huu unapanua ajenda za tafiti za programu za kondomu miongoni mwa ajenda zingine kama ifuatavyo:

- Ufuatiliaji wa masoko na tafiti katika sekta binafsi na za umma ili kutathimini ukuaji wa soko la jumla, pamoja na mienendo mingine, lengo ni kuleta mabadiliko ya programu thabiti kama inavyohitajika.
- Tafiti za matumizi, ikiwa ni pamoja na matumizi ya kondomu, tabia, ujuzi na mitazamo.
- Upatikanaji wa kondomu (ukaguzi wa masoko) kwenye sekta ya umma na binafsi.
- Utayari wa kulipia gharama za kondomu.
- Utambuzi wa makundi yasiyofikiwa kwa urahisi na huduma ya usambazaji wa kondomu
- Utambuzi wa vikwazo katika upataji na utumiaji wa kondomu kwa kulenga kondomu za kike.
- Upatikanaji wa tafiti na mbinu za usambazaji na mabadiliko ya kondomu, pamoja na athari zake.

Kunatakiwa kuwe na Ufuatiliaji na Tathmini thabiti ya programu za kondomu ili kuboresha ufikishaji na kutathimini ufanisi, pamoja na matokeo ya juu ya matumizi ya kondomu. Viashiria vyote muhimu vya taifa na dunia vinavyolenga makundi ya kawaida na maalumu yanapaswa kuzingatiwa sana. Vilevile, utunzaji wa kumbukumbu za michakato ya programu, maendeleo, na matokeo, sambamba na ugawaji wa hizi taarifa katika kuhakikisha kunakuwa na uwazi, uwajibikaji na ugawanyaji wa masomo unapaswa piakufanyika.

**Vipaumbele vya kimkakati:**

1. Kuboresha ufuatiliaji na tathmini ya programu za kondomu katika ngazi zote (Takwimu zinazohusu kondomu zinapaswa kuwa ni kipengele muhimu katika kufanya maamuzi, kama vile mahitaji, upatikanaji, Usambazaji.

[28] The national HIV/AIDS Research and Evaluation Agenda: 2011 - 2015

2. Kuimarisha tafiti za utekelezaji wa programu za kondomu.
3. Kujenga uwezo miongoni mwa wajumbe wa kamati mbalimbali za UKIMWI ili kuhakikisha utekelezaji fasaha wa programu za kondomu.

## SEHEMU YA 5: PROGRAMU ZA KONDOMU ZA KIKE NA AFUA ZA KIMKAKATI

### 5.1 Utangulizi

Kondomu za kike zilizinduliwa kwa mara ya kwanza nchini Tanzania mwaka 1998 na Shirika la Kimataifa linalohudumia Jamii kupitia masoko ya kijamii. Ili kuzuia unyanyapaa/ubaguzi juu ya kondomu ya kike, Shirika la Kimataifa linalohudumia Jamii liliinadi kama njia ya uzazi wa mpango, pamoja na kukinga magonjwa ya maaambukizo kupitia Ngono[29]. Shirika la Kimataifa linalohudumia Jamii nchini Tanzania liliinadi kondomu ya kike kama njia ya uzazi wa mpango kwa wanandoa waliohitaji kuzuia mimba zisizotarajiwa, pamoja na VVU. Ilijulikana kama "Care" ikiwa ni "Kwa wanandoa wanaojali". Kampeni zilizolenga wataalamu wenye kipato cha juu na cha kati zilitekelezwa mwaka 1999 kupitia vyombo vya habari, ili kuhamasisha matumizi ya kondomu ya kike. Kwa sababu za kufidia gharama, kondomu za kike ziliuzwa kwenye maduka ya Dawa baridi, Asasi za Kiraia, kwa watoa huduma za jamii na kwa mawakala wa kijamii.

Shirika la Masoko na Mawasiliano Tanzania lilitambulisha aina ya kondomu ya kike inayojulikana kama 'Lady Pepeta'. Soko lengwa la Lady Pepeta lilijumuisha hasa makundi yaliyo katika hatari, ikiwa ni pamoja na wanawake wanaofanya biashara ya ngono, wafanyakazi wa baa, na wanawake wanaojihusisha na ngono ya wapenzi wengi. Lady Pepepta inapatikana kupitia waelimishaji rika, wafanya biashara ya ngono na wafanyakazi wa baa ambao wamefunzwa kuwa mawakala wa mauzo.

Kwa sasa kondomu ya kike imeorodheshwa na Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba kama kifaa tiba. Shirika la Masoko na Mawasiliano Tanzania liiliwasilisha jalada la usajili la Kampuni ya uzalishaji wa kondomu ya kike na jina/nembo zinazounga mkono kondomu ya Lady Pepeta. Lady Pepeta ni kifaa tiba kilichosajiliwa kikamilifu nchini Tanzania na kabla ya usajili Lady Pepeta ilikuwa ikiingizwa/kusambazwa chini ya kibali cha msamaha wa bidhaa kilichokuwa kikitolewa na Shirika la Maendeleo la Marekani.

[29] Impact of Mass Media on Intention to Use the Female Conilidom, Sohail Agha and Ronan Van Rossem, 2002

Mfuko wa Umoja wa Mataifa wa Idadi ya Watu umetoa msaada kwa asasi ya kimataifa ya kudhibiti VVU na UKIMWI, uzazi wa mpango na afya ya uzazi ili kuhamasisha matumizi ya kondomu ya kike kwa kutumia ufumbuzi wa kisasa kama vile kutumia vielelezo rafiki katika kuonesha mfano kwenye baa na sehemu zenye mikusanyiko. Mbinu za Asasi ya kimataifa ya kudhibiti VVU na UKIMWI, uzazi wa mpango na afya ya uzazi zinalenga katika kunadi kondomu za kike na kuongeza kiwango cha ukubalikaji wa kondomu ya kike.

Mwaka 2007, utafiti ulifanyika katika Hospitali ya Mkoa ya Kagera ili kutambua kiwango cha ukubalikaji wa kondomu za kike kama njia ya kuzuia mimba baada ya mimba kutoka[30], ambapo kondomu za kike zilikubalika na watu 201 kati ya 521, ambayo ni sawa na asilimia 39, na ilitumika na watu 158 kati ya 521 ambayo ni sawa na asilimia 30. Wanawake waliotoa mimba isiyo salama, ni wale waliomaliza elimu ya sekondari au wenye kipato ambao wana uwezekano mkubwa wa kukubali kondomu za kike. Kwa ujumla, wanawake waliridhishwa na njia hii, na wengi wao walipanga kuitumia tena.

Mwaka 2013 Asasi ya kimataifa ya afya ya uzazi, kinga na huduma dhidi ya VVU na UKIMWI, pamoja na afya ya mama ilitumia nafasi ya upatikanaji usiotarajiwa/wa ghafla wa kiwango kikubwa cha kondomu za kike nchini Tanzania ili kuitambulisha kondomu ya kike miongoni mwa wateja wa programu za VVU/Uzazi wa Mpango.

### 5.2 Vikwazo katika kuongeza kiwango cha matumizi ya kondomu ya kike

- Kutokuwa na uwezo wa kumudu gharama za kununua kondomu kumeripotiwa katika tafiti nyingi, ikiambatanishwa na uwezo mdogo wa kujadili masuala yahusuyo ngono salama.
- Ukosefu wa ujuzi/uelewa juu ya namna ya kutumia kondomu ya kike.
- Ukosefu wa rasilimani watu wa kutosha wenye mafunzo ya jinsi ya kuonesha kwa mifano au kueneza ufanisi wa kondomu za kike kwa watumiaji, pamoja na ukosefu wa vifaa/vielelezo vya maonyesho.
- Fikra potofu juu ya matumizi ya kondomu za kike.
- Uwezo mdogo katika kujadiliana juu ya matumizi ya kondomu kwa wanawake.
- Matumizi mabaya ya kondomu za kike kwa madhumuni yasiyokusudiwa.

**30** Acceptance and use of the female condom among women with incomplete abortion in rural Tanzani, .Rasch V[1], Yambesi F, Kipingili R, 2007

### 5.3 Mikakati ya kuongeza kiwango cha matumizi ya kondomu ya kike

#### 5.3.1 Nafasi ya Kondomu ya Kike

Kondomu ya kike ni kukinga dhidi ya mimba zisizotarajiwa, maambukizi ya VVU na maambukizo mengine ya magonjwa kupitia ngono.

#### 5.3.2 Makundi Maalumu na Yaliyobainiwa

Kondomu ya kike ina uwezekano mkubwa wa kukinga maambukizi mapya kwa makundi lengwa/mahususi yakihusisha wanawake wanofanya biashara ya ngono na wateja wao, wanawake walio kwenye taasisi za elimu ya juu, wanandoa ambao mwenzi mmoja ana maambukizi ya VVU, (wakati mwenzi mwingine hana maambukizi), wanandoa ambao wote wana maambukizi, pamoja na wanawake na wanaume wasio na wenzi, wanaohitaji huduma.

#### 5.3.3 Njia mbalimbali za utoaji huduma na usambazaji

Programu za kondomu ya kike zinapaswa kutekelezwa kwa kutumia mbinu thabiti zinazojumuisha vituo vya sekta ya umma kama vile vituo vya afya, sekta binafsi (Maduka ya Dawa pamoja na maduka ya rejareja), masoko ya biashara jamii, pamoja na ushirikishwaji wa jamii katika maeneo ya vijijini na mijini

#### 5.3.4 Uimarishaji wa muunganisho wa Kondomu za Kike

Kwanza kabisa, mkakati upatikanaji wa kondomu za kike sambamba na zile kondomu za kiume. Kondomu za kike huonyesha mafanikio zaidi zinapounganishwa kwenye kinga dhidi ya VVU na Maambukizo wa Ngono na Huduma za Afya ya Jinsia na Uzazi

#### 5.4.5 Kuandaa mikakati bunifu ya uhamasishaji

Utafiti wa masoko utahitajika ili kutoa muongozo katika maendeleo ya mikakati inayohusiana na utamaduni mahususi/fasaha, mwitikio wa kijinsia, pamoja na masoko na mawasiliano mahususi. Mbinu za vyombo vya habari, msaada wa vijana rika na ushirikishwaji wa wanaume umebainiwa kuwa fasaha katika masoko ya kijamii ili kujenga uelewa/ujuzi, kushughulikia unyanyapaa na kuhamasisha mitazamo miongoni mwa watu. Hii inapaswa kuambatana na mawasiliano kati ya mtu na mtu kwenye vituo vya usambazaji kwa ajili ya kuonyesha mifano, kushika na kuihisi bidhaa, mafunzo juu ya matumizi sahihi, majadiliano juu ya mbinu katika makubaliano juu ya matumizi ya kondomu fursa ya kushughulikia maswali binafsi.

#### 5.4.6 Kutoa mafunzo kwa watoa huduma.

Ni muhimu kwamba watumiaji lengwa wanakuwa na uelewa juu ya nini cha kutegemea wakati wa majaribio yao ya kwanza ya kutumia kondomu ya kike, na wana ujasiri wa kutosha

wa kujaribu kuivaa na kuitumia hadi pale wanapokuwa wameridhika. Wauzaji wa kijamii wamefanikiwa kuwatumia wahamasishaji wa kondomu kwa kutumia kundi dogo na lenye mafunzo ya kutosha la wauzaji wanaotoa msaada wa kimkakati, ili kukuza na kuendeleza hamu ya mteja kwa kuhamasisha muunganisho wa kondomu, majadiliano na watoa huduma juu ya njia gani nzuri ya kuiweka kondomu kwa ajili ya makundi mbalimbali ya wateja, mafunzo ya wateja ya moja kwa moja, pamoja na kusaidia kwa usambazaji salama na wa kutosha.

### 5.4.7 Kufanya uraghibishaji wa Wadau Muhimu

Kuna aina mbalimbali za wadau waliobobea kwenye kufanikisha mipango, watekelezaji na wachukuaji wa kondomu ya kike: Mpango wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI na Asasi za kiraia, Viongozi wa kijiji, Viongozi katika ngazi ya wilaya, Viongozi wa dini, wanasiasa, WAVIU, watoa huduma, Makundi ya wanawake/watetezi wa haki za binadamu/mahakimu, Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala za Serikali na Wabia wa Maendeleo. Uhamasishaji wa wadau tajwa hapo juu unapaswa kufanyika ili kuinua rasilimali na kujenga umiliki wa programu za kondomu ya kike.

### 5.4.8 Kufanya Tafiti endeshaji za pamoja

Ili kuongeza uwezekano wa kupata mafanikio makubwa katika matumizi ya kondomu ya kike katika maeneo mengine, ni muhimu kufanya tafiti endeshaji ili kuelewa sababu za kijamii, kitamaduni, kiuchumi na kimuundo zinazohamasisha kutumia au kutotumia kondomu ya kike.

### 5.4.9 Kuandaa Msaada wa kitaalamu na kifedha

Rasilimali za kutosha zinapaswa kuandaliwa na kuelekezwa katika uandaaji, uuzaji na utekelezaji ili kuhakikisha kunakuwa na mafaniko katika majaribio, chini ya muongozo wa Kamati ya Usalama wa bidhaa za Afya ya Uzazi.

## SEHEMU YA 6: MAJUKUMU NA WAJIBU WA WADAU MUHIMU

Taasisi za Kiserikali kulingana na wajibu na majukumu yao zitagawana wajibu, majukumu na usimamizi wa program za kondomu zenye kuleta tija na ufanisi. Kwa kuzingatia mamlaka za taasisi hizo, kuna uwezekano wa majukumu yanayofanana kujikita sehemu moja, hivyo kamati Ndogo ya Kondomu ya Kitaifa itakuwa na wajibu wa kuyaoanisha. Majukumu ya kila mdau yameorodheshwa kama ifuatavyo:

### 6.1 Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS)

Tume inaendesha shughuli zake za Utawala, Uangalizi na uratibu kutoka katika kifungu cha sheria NA. 22 cha mwaka 2001.Tume inaendesha shughuli zake chini ya mamlaka ya Ofisi ya Waziri Mkuu; inaelekeza Mwitikio wa Taifa wa VVU na UKIMWI, na uratibu wa sekta zote ambao ni muhimu kwa kuunganisha wadau wa kiserikali na wasio wa kiserikali. Aidha, Tume ina wajibu wa kimkakati katika kuongoza na kuratibu utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI (IV), uraghibishi, utafutaji na ugawaji wa raslimali fedha. Pia, Tume ina wajibu wa kuoanisha mifumo ya habari ili kupata viwango vya juu vya taarifa ya viashiaria vya Mkakati wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI, pamoja na kuyaelekeza makundi kazi ya kitaalamu katika kuhakikisha kunakuwa na mawasiliano kati ya wadau na uwajibikaji katika matokeo. Tume itatimiza majukumu yafuatayo katika utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Kondomu:

- Utafutaji ya rasilimali.
- Uraghibishi katika ngazi ya Sera na Wizara.
- Kuongoza na kuratibu mwitikio wa VVU kwenye sekta za Wizara, Idara Zinazojitegema na Wakala wa Serikali, Asasi za Kiraia na kijamii, na sekta binafsi/zisizo rasmi.
- Usambazaji wa Mkakati wa Taifa wa Kondomu.

### 6.2 WIZARA, IDARA ZINAZOJITEGEMEA NA WAKALAWA SERIKALI

Wajibu na majukumu ya Wizara, Idara Zinaojitegemea na Wakala za Serikali yanayohusiana na programu za kina za kondomu ni pamoja na:

- Utafutaji wa rasilimali.
- Uraghibishi.
- Uhamasishaji wa jamii juu ya ufanisi wa kondomu
- Usambazaji endelevu wa kondomu katika makundi yaliyotambulika katika ngazi ya Kanda, ya wilaya na jamii.

### 6.3 Wizara ya Afya , Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto

Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kupitia Mpango wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI na Huduma ya Afya ya uzazi na mtoto itakuwa na mchango kwa vituo vya afya, wafanyakazi wa huduma ya afya, na maafisa wa ustawi wa jamii wanaopokea miongozo ya kitaalamu kutoka wizarani. Vilevile, Sekta ya Maendeleo ya Jamii itachangia katika eneo hili la uwekezaji, ikilenga mazingira ya kijamii na kitamaduni yaliyopo katika jamii ya Tanzania yanayoweka watu katika mazingira hatarishi ya kupata maambukizi ya VVU, pamoja na kuwaweka WAVIU katika mazingira hatarishi ya kutopata huduma za kiuchumi na kiafya. Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto itatimiza majukumu yafuatayo:

- Utafutaji wa rasilimali.
- Uraghibishi/Utekelezaji wa Mkakati wa Kondomu kupitia Mpango wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI na Huduma ya Afya ya uzazi na mtoto
- Usambazaji wa mwongozo wa usambazaji wa kondomu kupitia Mpango wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI.
- Mipango ya makadirio na manunuzi ya kondomu.
- Usambazaji wa Kondomu zenye nembo/jina za sekta ya umma kwa makundi maalumu na yaliyo katika mazingira hatarishi.
- Kutoa muongozo kwa Asasi zisizo za kiserikali katika utekelezaji wa makakati wa kondomu.
- Uendeshaji wa mfumo wa ufuatiliaji na tathmini katika program za kondomu.
- Kuhakikisha kunakuwa na upatikanaji wa kondomu katika sekta ya umma.

### 6.4 Elimu na Mafunzo ya Ufundi

Wizara, Idara Zinazojitegemea na Wakala za Serikali wanaohusika na elimu wana wajibu wa kuchangia katika mwitikio wa taifa wa VVU na UKIMWI kupitia utoaji wa elimu ya msingi, stadi za maisha na mafunzo maalumu ya kitaalamu. Elimu ya kina ya jinsia, jinsi, na afya katika ngazi ya shule za msingi, sekondari na elimu ya juu, pamoja na nje ya mazingira ya shule, ni uwekezaji wa kipaumbele katika kuwawezesha WAVIU kuishi bila woga wa unyanyapaa na ubaguzi. Yafuatayo ni majukumu na wajibu wao katika utekelezaji wa Mkakati wa Kondomu:

- Kuhakikisha kwamba kondomu ni sehemu ya mtaala wa kina wa jinsia.
- Kuhamasisha tabia chanya juu ya matumizi ya kondomu.
- Kuhakikisha upatikanaji wa kondomu kwa vijana wenye umri wa miaka kati ya 15-24 walio ndani na nje ya shule.

### 6.5 Wizara ya fedha na Mipango

Wizara ya Fedha na Mipango ina wajibu wa kusimamia mahesabu/fedha ya mwitikio wa taifa katika masuala ya VVU na UKIMWI. Chombo hiki kina majukumu ya kupanga na kutoa fedha kwa ajili ya VVU na UKIMWI kwa taasisi zinazohusika na utekelezaji wa mkakati wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI. Kwa upande wa programu ya kondomu, watawajibika katika upangaji na ugawanyaji wa rasilimali.

### 6.6 Mamlaka ya Serikali za Mtaa

Sambamba na sera za serikali katika mgawanyiko wa madaraka katika makabidhiano ya madaraka., Mkakati wa kondomu unaongeza msisitizo katika uwajibikaji nakuimarisha usambazaji na upatikanaji wa kondomu katika ngazi ya mamlaka ya Serikali za Mitaa. Mfumo wa Mamlaka za Serikali za Mitaa unajumuisha; Kamati za Kudhibiti UKIMWI za Viijiji/Mitaa, Kamati za Kudhibiti UKIMWI za Kata, Kamati za Kudhibiti UKIMWI za Halmashauri za Wilaya, Waratibu wa VVU na UKIMWI wa Halmashauri ya Wilaya, Waratibu wa Kudhibiti UKIMWI wa Wilaya; Wafamasia wa Wilaya, Wakuu wa Wilaya na Kamati za Ushauri za Wilaya ambazo ni nyenzo muhimu katika mipango na utelekezaji wa program za VVU. Utekelezaji wa mkakati wa program za kondomu unahitaji mawasiliano thabiti, pamoja na ushirikiano katika kila ngazi ili kuhakikisha kwamba kondomu zinawafikia watumiaji lengwa. Waratibu wa TACAIDS wa Mkoa watawajibika na ugawaji wa mkakati wa kondomu katika ngazi ya Mkoa.

### 6.7 Wizara zingine, pamoja na Idara Zinazojitegemea Wakala za Serikali

Wizara zingine zote, pamoja na Idara zinazojitegemea na Wakala za Serikali wana wajibu wa kuhakikisha kwamba sehemu za kazi zina sera mahususi kwa ajili ya WAVIU na ambazo zinatelekezwa kwa ufasaha. Hizi ni pamoja na juhudi za pamoja kati ya waajiri wa sekta za umma na za binafsi, pamoja na taasisi zinahusu bima yenye uhakika ya ulemavu kwa WAVIU. Yafuatayo yatakuwa ni majukumu yao yanayohusu programu za kondomu:

- Kufanya tathmini ya matumizi ya kondomu miongoni mwa waajiriwa na wateja wao kadri itakavyowezekana
- Kuhakikisha kunakuwa na upatikanaji na matumizi ya kondomu miongoni mwa waajiriwa na watu wanaowahudumia
- Kutoa mafunzo kwa waajiriwa ikiwa ni pamoja na mitandao m.f Madereva wa masafa, marefu, Wachimbaji wa madini, wafanyabiashara ya ngono n.k.

### 6.8 Utafiti na Taasisi za Elimu ya Juu

Taasisi za Elimu ya Juu zinawajibika ipasavyo katika Mwitikio wa taifa wa VVU na UKIMWI, kupitia muongozo wa kitaalamu, tafiti na mafunzo ya wataalamu wa baadae. Ujumuishaji wa maarifa kuhusu matumizi ya kondomu katika mipango anuai yakitaaluma inapaswa kutekelezwa.

### 6.9 Sekta binafsi rasmi na zisizo rasmi

Sekta binafsi rasmi nchini Tanzania inaratibiwa kupitia Chama cha Waajiri Tanzania kwa kushirikina na Mfuko wa Sekta Binafsi Tanzania. Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania pamoja na Wizara ya Kazi ziliunda shirika mwamvuli kutengeneza ubia sekta za umma na binafsi. Chama cha waajiri Tanzania inajumuisha makampuni zaidi ya 800 (makampuni madogo, ya kati na makubwa). Kwa upande wa sekta zisizo rasmi, Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania itashirikiana na Mitandao ya Uchumi isiyo Rasmi Kuhusu Mapambano dhidi ya UKIMWI Tanzania (TIENAI) kulifufua tena hili kundi kwa vile linajumuisha wajumbe wengi katika jamii. Kupitia uwajibikaji wa pamoja kijamii, sekta binafsi (rasmi na zisizo rasmi) zinapaswa kutayarisha mikakati ya kutoa elimu juu ya matumizi ya kondomu, ununuzi na usambazaji wa kondomu miongoni mwa nguvu kazi kwa kutumia mashine za kuweka na kutoa kondomu katika sehemu zote za kazi.

### 6.10 Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba

Ubora wa kondomu ni muhimu sana kwa mafanikio ya program za kondomu. *Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba* ni taasisi yenye mamlaka ya kuhakikisha kwamba ubora wa kondomu unaingia kwenye Mfumo wa huduma za afya. Mawakala wataendelea kuhudhuria mikutano ya kamati shirikishi za taifa za kondomu na kutoa muongozo unaohusu masuala ya ubora wa kondomu.

### 6.11 Wabia wa Maendeleo

Wadau muhimu wa maendeleo watachangia kwenye programu za kondomu kwa kutoa misaada kwa asasi za kijamii za masoko ya manunuzi ya kondomu kwa sekta za umma na binafsi (binafsi yasiyotengeneza faida na masoko ya jamii).

### 6.12 Asasi za Kiraia na Kijamii

Asasi za Kiraia na Kijamii zina majukumu anuai kwenye mipango ya programu za kondomu zikiwemo sekta za masoko ya kijamii, pamoja na uungwaji na ushirikishwaji wa jamii. Sekta za masoko ya kijamii zinasaidia kuongeza kiwango cha uhitaji wa kondomu na kupunguza vikwazo vinavyohusiana na fursa, uwezo na hamasa katika kutumia kondomu. Vilevile, sekta

ya masoko ya kijamii inatoa msaada wa kitaalamu kwa sekta za umma ili kufuatilia na kuteka soko zima la kondomu.

### 6.13 Shirika la Sekta Binafsi ya Afya Tanzania

Shirikisho la Vituo Binafsi vya Afya Tanzania ni Shirika mwavuli la sekta binafsi ya afya inayotoa utetezi fasaha na wa kina, utawala, kushirikiana ujuzi na mtandao wa bidhaa na huduma. Shirikisho la Vituo Binafsi vya Afya Tanzania ina zaidi ya wanachama 10,000 Vituo vya afya, Maduka ya Dawa Baridi, na Maabara binafsi. Kupitia vituo binafsi vya afya, mbinu zinapaswa kutumika ili kuhakikisha kuwa ushiriki wao kamili katika programu za kondomu unajumuisha utoaji wa elimu juu ya matumizi ya kondomu, ununuzi na usambazaji wa kondomu katika jamii.

## REFERENCES


1) Acceptance and use of the female condom among women with incomplete abortion in rural Tanzania, .Rasch V[1], Yambesi F, Kipingili R, 2007
2) Global AIDS response progressing report (GARPR), 2012
3) Health Sector HIV and AIDS Strategic Plan IV 2017-2022
4) HIV and STI Biological and Behavioral survey,2013
5) HIV and AIDS Prevention and Control Act, (HAPCA) 2008
6) http://www.who.int/hiv/topics/condoms/en/
7) http://www.who.int/hiv/topics/condoms/en/
8) Impact of Mass Media on Intention to Use the Female Condom, Sohail Agha and Ronan Van Rossem, 2002
9) Mann Global Health: Tanzania Case Study; 2018
10) Measure Access and Performance of Fast Moving Consumer Goods report, PSI 2014
11) Ministry of Health and Social Welfare, a report of the controller and auditor general of the United Republic of Tanzania, National HIV and AIDS response report 2012, Tanzania mainland
12) National Condom Distribution Guideline 2019, NACP
13) National Family Planning Costed Implementation Plan, 2019-2013
14) National Guideline for Comprehensive Package of HIV in Interventions for Key Populations, 2014
15) National Guidelines for Initiating and Managing Community Based Reproductive and Child Health Services, Reproductive and Child Health Section
16) National guidelines for the Management of HIV and AIDS, NACP 2012
17) National Policy on HIV/AIDS, 2001
18) Needscope 2013
19) Omnibus results PSI-Tanzania 2014
20) Quantification of Reproductive, Maternal and Child Health Commodities for Mainland Tanzania, Forecasts for the period January 2019 to December 2020
21) *Social Marketing Evolves to Achieve Total Market Development and Sustainable Health Impact;* Reed Ramlow, Project Director, USAID Global Private Sector Program, AED Center for Private Sector Health Initiatives
22) Spectrum,2013
23) Tanzania Demographic Health Survey and Malaria Indicator Survey 2015-2016
24) TANZFIGURES 2012, National Bureau of Statistics, Ministry of Finance, June, 2013

25) Tanzania HIV/AIDS and Malaria Indicator Survey 2011-12
26) Tanzania HIV Impact Survey 2016-2017
27) The National HIV/AIDS Research and Evaluation Agenda: 2011 – 2015
28) Tanzania Global Health Initiative Strategy 2010 -2015
29) Gissenge L.I. Lija et al: Condom Distribution: Assessment of the Availability and accessibility in the Selected Hotspots of Dar es Salaam, Mwanza and Mbeya Cities, Tanzania
30) Tanzania (2009): Map Study on Market Penetration of Condoms. Round four. PSI Tanzania
31) Tanzania (2008) – Market penetration of condoms study. Third round, PSI Tanzania
32) Tanzania Third National Multi-Sectoral Strategic Framework for HIV and AIDS (2013/14 – 2017/18)
33) Total Market Approach Research: Retail Audit Study by SHOPS PLUS 2019
34) www.mannglobalhealth.com

**KIAMBATISHO CHA 1: Kiwango cha kondomu zinazohitajika Tanzania 2019-2020**

Ili kupata hesabu ya idadi ya kondomu zinazohitajika nchini Tanzania, Uhitaji kwa wote, usambazaji na mgawanyo wa masoko ulizingatiwa. "Uhitaji kwa wote" ni makadirio ya idadi ya kondomu zinazohitajika katika kujikinga dhidi ya VVU na mimba zisizotarajiwa kwa asilimia 100. Katika kulisogeza soko karibu ili kukidhi lengo la uhitaji kwa wote, ni lazima usambazaji na uhitaji ukue.

**Uhitaji kwa wote:**

Uhitaji kwa Wote ni idadi ya kondomu zinazohitajika kwa mwaka. Kiwango cha uhitaji kwa wote kilikadiriwa kuwa chini kwa makundi mawili:

- Wanaume wanaofanya ngono zembe/hatari (wenye kinga na wasiotumia kinga) Utafiti wa Viashirio vya VVU NA UKIMWI na Malaria Tanzania ya mwaka 2011/12 ilidhihirisha kwamba asilimia 20.8 ya wanaume (miaka 15-49) waliripotiwa kuwa na wapenzi wengi katika kipindi cha miezi 12 iliyopita;
- Asilimia 2.7 ya wanawake walio katika umri wa kuzaa (miaka 15-49) ambao waliripotiwa kutumia kondomu kama njia ya uzazi wa mpano (DHIS)

Jedwali la 5: linaonyesha makadilio ya idadi ya kondomu zinazohitajika Tanzania mwaka 2019-2025

| **Makisio yaliyotumika katika kutoa hesabu ya idadi ya kondomu za kike kwenye afya ya umma** | **Mkadirio ya kiwango cha ongezeko katika makundi (%)** | **2.82 (2020 makadirio.)** | **2.82% (2021 makadirio.)** | **2.82% (2022 makadirio.)** | **2.82% (2023 makadirio.)** | **2.82% (2024 est.)** | **2.82% (2025 est.)** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **2019** | **2020** | **2021** | **2022** | **2023** | **2024** | **2025** |
| Idadi ya kundi la wanaume (miaka 15-49.) Chanzo: Sensa ya mwaka 2012 | **11,242,692** | **11,242,692** | **11,559,736** | **11,885,721** | **12,220,898** | **12,565,527** | **12,919,875** |
| Kundi la wanaume lililo katika hatari kubwa | **2,211,966** | **2,274,344** | **2,338,480** | **2,404,425** | **2,466,803** | | |

| **Makisio yaliyotumika katika kutoa hesabu ya idadi ya kondomu za kike kwenye afya ya umma** | **Mkadirio ya kiwango cha ongezeko katika makundi (%)** | **2.82 (2020 makadirio.)** | **2.82% (2021 makadirio.)** | **2.82% (2022 makadirio.)** | **2.82% (2023 makadirio.)** | **2.82% (2024 est.)** | **2.82% (2025 est.)** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **2019** | **2020** | **2021** | **2022** | **2023** | **2024** | **2025** |
| (asilimia 20.8% ya kundi lenye umri wa miaka 15-49) chano: THMIS 2011/12 | | | | | | | |
| Kufikia lengo (asilimia 70%) Kundi | - | - | - | 1,548,376 | 1,592,040 | 1,636,936 | 1,683,098 |

| **Makisio yaliyotumika katika kutoa hesabu ya idadi ya kondomu za kike kwenye afya ya umma** | **Mkadirio ya kiwango cha ongezeko katika makundi (%)** | **2.82 (2020 makadirio.)** | **2.82% (2021 makadirio.)** | **2.82% (2022 makadirio.)** | **2.82% (2023 makadirio.)** | **2.82% (2024 est.)** | **2.82% (2025 est.)** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **2019** | **2020** | **2021** | **2022** | **2023** | **2024** | **2025** |
| lililo katika hatari kubwa zaidi lenye umri wa miaka 15-49 (HSSP III 2013 - 2017) | | | | | | | |
| Idadi ya kondomu kwa mtu mmoja kwa wiki | - | - | - | 3 | 3 | 3 | 3 |

| **Makisio yaliyotumika katika kutoa hesabu ya idadi ya kondomu za kike kwenye afya ya umma** | **Mkadirio ya kiwango cha ongezeko katika makundi (%)** | **2.82 (2020 makadirio.)** | **2.82% (2021 makadirio.)** | **2.82% (2022 makadirio.)** | **2.82% (2023 makadirio.)** | **2.82% (2024 est.)** | **2.82% (2025 est.)** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **2019** | **2020** | **2021** | **2022** | **2023** | **2024** | **2025** |
| Mahitaji ya kondomu kwa mwaka | - | - | - | 241,546,696 | 248,358,313 | 255,362,018 | 262,563,226 |
| Jumla ya kondomu zinazohitajika kwa mwaka | - | - | - | 241,546,696 | 248,358,313 | 255,362,018 | 262,563,226 |
| Kondomu za kike za RCHS Male condoms | - | - | - | - | 35,491,050 | 38,011,421 | 38,011,421 |

| **Makisio yaliyotumika katika kutoa hesabu ya idadi ya kondomu za kike kwenye afya ya umma** | **Mkadirio ya kiwango cha ongezeko katika makundi (%)** | **2.82 (2020 makadirio.)** | **2.82% (2021 makadirio.)** | **2.82% (2022 makadirio.)** | **2.82% (2023 makadirio.)** | **2.82% (2024 est.)** | **2.82% (2025 est.)** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **2019** | **2020** | **2021** | **2022** | **2023** | **2024** | **2025** |
| (umma + masoko ya kijamii + biashara) | | | | | | | |
| Jumla ya kondomu zinazohitajika katika nchi (umma + masoko ya kijamii + biashara) | **-** | **-** | | | 283,849,363 | 293,373,439 | 300,574,647 |

| **Makisio yaliyotumika katika kutoa hesabu ya idadi ya kondomu za kike kwenye afya ya umma** | **Mkadirio ya kiwango cha ongezeko katika makundi (%)** | **2.82 (2020 makadirio.)** | **2.82% (2021 makadirio.)** | **2.82% (2022 makadirio.)** | **2.82% (2023 makadirio.)** | **2.82% (2024 est.)** | **2.82% (2025 est.)** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **2019** | **2020** | **2021** | **2022** | **2023** | **2024** | **2025** |
| Mchango wa kondomu katika sekta ya umma (asilimia 50) | - | - | - | 41,062,938 | 141,924,681 | 146,686,719 | 150,287,324 |
| Idadi ya kondomu zinazohitajika kwa mwaka | - | | | **41,062,938** | **141,924,681** | **146,686,719** | **150,287,324** |

| **Makisio yaliyotumika katika kutoa hesabu ya idadi ya kondomu za kike kwenye afya ya umma** | **Mkadirio ya kiwango cha ongezeko katika makundi (%)** | **2.82 (2020 makadirio.)** | **2.82% (2021 makadirio.)** | **2.82% (2022 makadirio.)** | **2.82% (2023 makadirio.)** | **2.82% (2024 est.)** | **2.82% (2025 est.)** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **2019** | **2020** | **2021** | **2022** | **2023** | **2024** | **2025** |
| Makadirio ya kondomu katika AMC kwa mwaka (kila mwezi) | **-** | | | **-** | **11,827,056.78** | **12,223,893.28** | **12,523,943.64** |

**NK:** Mahesabu ya kondomu zinazohitajika yatafanyika kila baada ya miaka miwili kutegemea na ongezeko la watu